# Nipashe

Jumamosi Aprili 29, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581295

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710

LIKE & FOLLOW US




UKURASA 11

SUPA JACKPOT

TZS. 1,107,465,397

KWA TZS. 1000 TU!

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SportPesa.CO.TZ

PIGA *150*87#



## Tahadhari mvua kubwa mikoa ya Pwani, Zanzibar

UKURASA 3



# MSHTUKO

• **Takwimu** ushoga zatisha, shule awali, NGO zahusishwa, Padri awaonya wanandoa ...*Endelea Ukurasa 2 & 15*

UKURASA WA 2

## MUUGUZI ASIMAMISHWA KAZI KWA MADAI KUFANYA UPASUAJI

BARAZA la Uuguzi na Ukunga Tanzania (TNMC), limemsimamisha kazi miezi sita Ofisa Muuguzi Msaidizi Paul Urio, kwa kosa la kushindwa kusimamia viwango vya maadili kitaaluma...

## Vuta nikuvute wauza magazeti kuporwa meza na mgambo wa jiji

UKURASA 3



Rais Samia Suluhu Hassan akizungumza na wageni mbalimbali waliofika kwenye dhifa ya kitaifa aliyomwandalia mgeni wake, Rais wa Rwanda, Paul Kagame (wa pili kushoto), Ikulu jijini Dar es Salaam juzi jioni. Kushoto ni Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Dk. Stergomena Tax. **PICHA: IKULU**



## Utaratibu wa uuzaji tanzanite maeneo ya awali kurejeshwa

UK. 2

**MICHEZO** RAIS DK. SAMIA AONGEZA DAU UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6



Wanafunzi wa Shule ya Sekondari Dodoma, wakitoa elimu ya jinsi ya kuondoa sumu iliyoathiri maini ya binadamu kutokana na unywaji wa pombe na uvutaji wa sigara, wakati wa maonyesho ya ubunifu, jijini Dodoma juzi. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Mshtuko takwimu za ushoga zatisha

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

Ni mshtuko. Ndivyo ambavyo inaweza kuelezwa kutokana na takwimu za vitendo vya ushoga vilivyoibuliwa ndani ya wilaya ya Arusha huku shule za awali na mashirika yasiyo ya kiserikali yakidaiwa kuwa ni chanzo kikuu.

Hayo yalibainishwa na Mkuu wa Wilaya ya Arusha, Felician Mtehengerwa, ambaye amesema hali ya ushoga katika Jiji la Arusha ni mbaya na kwamba inakadiriwa zaidi ya vijana 4,000 wamebainika kujihusisha na mapenzi ya jinsia moja.

Mtahengerwa alifichua hilo jana, wakati alipopewa nafasi ya kuzungumza katika kikao cha Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Jiji la Arusha.

Kutokana na ongezeko la vitendo hivyo, Mkuu huyo aliwasihi madiwani wa Jiji la Arusha kujitosa katika vita hivyo kwenye maeneo yao.

Alisema baadhi ya maeneo ambayo yanatajwa kushamiri kwa vitendo hivyo ni shule za awali (Day Care) na baadhi ya taasisi za kijamii (NGO) ambazo zinaomba usajili kwa minajili ya kutoa elimu kwa jamii.

Kwa mujibu wa mkuu huyo, taarifa alizo nazo ni kwamba kuna taasisi nyingine zinakuja kwa mgongo wa kutoa elimu kwa wananchi kumbe zinaratibu masuala ya ushoga kupitia shule za awali na katika vituo vya taasisi zao.

Alisema mtu huyo tayari wanamshikilia baada ya kukamatwa akiwa anasajili taasisi kwa minajili ya kutoa elimu ya ushoga. "Ukiambiwa idadi ya mashoga hapa Arusha utashika kichwa. Ni zaidi ya vijana 4,000 kwa takwimu alizo nazo huyu aliyekamatwa na wengi ni watoto wetu. Hali ni mbaya, tuchukue hatua za udhibiti mwenendo wao," aliomba.

Kwa mujibu wa Mtahengerwa, kuna fedha nyingi zinatolewa kwa shule binafsi na taasisi za kijamii, kuratibu na kufundisha mapenzi ya jinsia moja na walipoulizwa walidai wanatoa elimu kwa watu hao ili kutambua hali zao.

"Juzi kuna mtu mmoja alibainika kusajili taasisi ya kijamii, tulipoifuatilia tumegundua kibali amedanganya, na pia taasisi hiyo inajihusisha na vitendo vya kuwafundisha vijana mapenzi ya jinsia moja," alisema.

Aliwataka madiwani hao kuchukuwa hatua za kukemea vitendo hivyo kwa kuongea na wananchi wa maeneo yao, ili kuwafuatilia matendo ya watoto wao wanakwenda na kurudi nyumbani.

"Niwaombe wazazi fuatilieni mienendo na muwakague wanaume zenu na watoto wenu hali ni mbay,a haiwezekani mtoto anatoka hovyo bila kuaga na kurudi, mzazi hujuwi mienendo yake, hili hata sisi kwenye makuzi hatukulelewa hivyo," alisema.

Mutahengerwa alisema wazazi waliwafuatilia ndio maana vitendo viovu havikuwapo kwa kasi kama sasa ambapo kila siku wanapokea ripoti ya watoto wawili kulawitiwa.

Alisema wameshaanza mapambano ya kukabiliana na vitendo hivyo na kuwaomba madiwani ushirikiano kwenye mapambano hayo, kwa kuwa zilizomwagwa kwenye ushoga ni nyingi, wakati kuna mambo mengi ya miradi ya maendeleo.

# Utaratibu uuzaji tanzanite maeneo ya awali kurejeshwa

**Na Gwamaka Alipipi,** DODOMA

SERIKALI inatarajia kurejesha utaratibu wa kufanyika kwa minada ya madini ya tanzanite katika maeneo ya awali pamoja na maonyesho ya madini ya vito, imeelezwa.

Waziri wa Madini, Dk. Doto Biteko, aliyasema hayo jana bungeni jijini Dodoma wakati akijibu hoja za baadhi ya wabunge waliochangia makadirio ya mapato na matumizi kwa wizara yake kwa mwaka 2023/24, ikiwamo urejeshaji wa minada ya uuzaji wa tanzanite katika maeneo ya awali.

Mwaka 2017, serikali iliagiza uuzaji wa tanzanite kufanyika Mji Mdogo wa Mirerani, Simanjiro mkoani Manyara, lengo likiwa ni kudhibiti utoroshaji wa madini hayo kwenda nje ya nchi, kuongeza mapato. Hatua hiyo ililazimu serikali kujenga ukuta eneo hilo sambamba na kufunga kamera ili kudhibiti utoroshaji.

Akijibu hoja za wabunge jana, Biteko alisema: "Baadhi ya wabunge akiwamo Mrisho Gambo, wamezungumzia kuhusu kubadilisha kanuni ya Mirerani controlled Area ambayo ilikuwa inaagiza minada ya madini kufanyika Mirerani pekee. Lengo la serikali lilikuwa ni kuifanya Mirerani kuwa eneo la kuchangamka.

"Rais Samia Suluhu Hassan ameshatupa maelekezo na tumeshalisikia na tumeanza kulifanyia kazi, napenda kuwaambia kuwa tutarejesha minada ya madini, maonyesho ya madini ya vito nchini kama ilivyokuwa huko awali."

Biteko alisema serikali iliacha kufanya hivyo mwaka 2017, kwamba kuanzia sasa taratibu za kurejesha minada hiyo maeneo ya awali unafanyika. "Hivi ninavyozungumza kuna timu ya wataalamu ambayo imekwenda kuangalia namna minada mingine inavyofanyika katika nchi mbalimbali ikiwamo ya Thailand. Wanaoendesha minada nje ya nchi wamekubali kuja nchini kutuendeshea minada kwa bei nzuri kwa wachimbaji," alisema.

Kuhusu wachimbaji wadogo kufukuzwa katika maeneo yenye migogoro, Biteko alisema tangu Rais Samia alipoingia madarakani hakuna mchimbaji mdogo aliyefukuzwa katika maeneo ya uchimbaji.

Alisema maeneo ambayo wachimbaji wadogo wanasimamishwa kuchimba ni yake yanye masuala ya usalama.

Waziri Biteko alitoa mfano kwa wachimbaji wa madini wa eneo la Kinyambwiga akisema isingekuwa vizuri kuendelea kuruhusu waendelee kuchimba kwa sababu kulikuwa na vurugu.

"Ni eneo ambalo watu wenyewe walitaka kuonyesha wana nguvu kuliko wasimamizi, tulipeleka polisi alipigwa, tulipela walinzi walipigwa, hatua ya kwanza tuliamua kurejesha amani kwa kusimamisha uchimbaji na baada ya hali kutulia tulirudisha shughuli za uchimbaji," alisema.

# Muuguzi asimamishwa madai kufanya upasuaji

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

BARAZA la Uuguzi na Ukunga Tanzania (TNMC), limemsimamisha kazi miezi sita Ofisa Muuguzi Msaidizi Paul Urio, kwa kosa la kushindwa kusimamia viwango vya maadili kitaaluma.

Ofisa huyo anadaiwa kukiuka kifungu cha 25(3) (k) cha Sheria ya Uuguzi na Ukunga ya mwaka 2010 kwa kutoa huduma bila kufuata miongozo ya afya.

Shauri hilo Na. 4 la mwaka 2023, lilisikilizwa juzi jijini hapa na Mwendesha Mashtaka Mkuu wa Serikali, Catherine Gwaltu, kutoka Ofisi ya Mashtaka Mkoa wa Dodoma.

Muuguzi huyo alishtakiwa kwa kushindwa kusimamia viwango vya kitaaluma na maadili ya uuguzi na ukunga kinyume na kifungu cha 25(3) (k) cha Sheria ya Uuguzi na Ukunga Tanzania ya mwaka 2010.

Inadaiwa kuwa Desemba 2, mwaka jana, akiwa Ofisa Muuguzi Msaidizi aliingia kazini katika kituo cha afya Usa River, Halmashauri ya Arumeru mkoani Arusha na kufanya upasuaji wa Hernis (Hernioraphy) kwa mgonjwa Daudi Denis kinyume cha taratibu na kumsababishia madhara ya kiafya.

Pia anadaiwa kuchukua fedha iliyopaswa kulipwa kwa kituo cha afya kwa matumizi yake binafsi kinyume cha kifungu cha 25(3) (g) cha Sheria ya Uuguzi na Ukunga Tanzania ya mwaka, 2010.

Pia siku ya tukio, inadaiwa kuwa aliingia kazini katika kituo hicho cha afya na kuchukua fedha kutoka kwa mgonjwa ili kufanyiwa upasuaji, fedha zilizopaswa kulipwa kwa kituo cha afya Usa River lakini alizitumia kwa matumizi yake binafsi. Baada ya kusomewa mashitaka yanayomkabili, Urio alikana kutenda tuhuma zilizomkabili.

Kutokana na hali hiyo, Baraza liliwaita mashaidi kutoa ushahidi ambapo mtu wa kwanza alikuwa Dk. John Ngowi.

Baada ya kusomewa mashtaka yanayomkabili chini ya kifungu 25(3) (k) na 25 (3) (g) cha ya sheria ya uuguzi na ukunga ya mwaka 2010 na kusomewa maelezo ya kosa linalomkabili kusikiliza mashahidi.

Mwenyekiti wa baraza hilo, Prof. Lilian Mselle alimweleza kuwa baraza limemtia hatiani kwa kosa la kwanza la kushindwa kusimamia viwango vya maadili.

"Baraza halikukutia hatiani kwa kosa la pili chini ya kifungu 25(3) (g) sheria ya uuguzi na ukunga Tanzania ya mwaka 2010, baraza linakupa fursa ya kujitetea kabla ya kutoa adhabu.

"Baada ya kusikiliza utetezi wako, baraza linakusimamisha kutoa huduma za uuguzi na ukunga kwa muda wa miezi mitatu chini ya kifungu 28 (3) (b) cha sheria ya uuguzi na ukunga ya mwaka 2010," alielezwa.

Alisema katika kipindi hicho, muuguzi huyo hataruhusiwa kutoa huduma yoyote ya uuguzi na ukunga pamoja na za ganzi na usingizi na asiporidhika ana haki ya kukata rufani.

# Vuta nikuvute wauza magazeti kuporwa meza na mgambo wa jiji

**Na Maulid Mmbaga**

SINTOFAHAMU imeibuka kwa wauza magazeti wa eneo la Posta jijini Dar es Salaam, baada ya meza zao kuchukuliwa na askari wa jiji waliodai kuwa wamepewa maagizo hayo na Ofisa Utumishi wa Jiji la Dar es Salaam kwamba ni maelekezo kutoka Ofisi ya Mkuu wa Mkoa.

Nipashe ilipomtafuta jana Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makala, ili kuzungumzia kuhusu hilo, alikanusha kutoa maagizo hayo na kusema hana taarifa zozote kuhusu suala hilo.

Operesheni ya kuwapanga wafanyabiashara kwa lengo la kupendezesha mkoa huo ilipofanyika awali, wauzaji wa magazeti waliruhusiwa kuweka meza zao katika maeneo waliyopewa kwa masharti ya kutokuchanganya na bidhaa zingine.

Gazeti hili lilibaini jana kuwa meza za wauza magazeti hao zilichukuliwa juzi jioni na kupelekwa kwenye karakana ya Kamata, jambo lililosababisha hasara kwa kampuni za magazeti na kwa wauzaji hao kutokana na kushindwa kuendelea na biashara.

Makalla alisema huenda kuna jambo limetokea ndio maana watu hao wamefanya hivyo, lakini yeye binafsi hana taarifa zozote kuhusu suala hilo.

Alisisitiza kwamba upangaji wa wafanyabiashara ulifanyika muda mrefu kwa ajili ya kulipendezesha jiji na kwamba wa wauzaji wa magazeti walipatiwa maeneo yao wanayoyatumia kuendesha shughuli zao.

Kiongozi huyo ameonyesha kushangazwa na taarifa ya kwamba yeye ndiye aliyetoa maagizo ya meza hizo kuondolewa.

"Siku zote wauza magazeti walikuwa katika maeneo yao. Kwa nini leo (jana) ndio waondolewe?. Labda suala hilo lilianzia ngazi za chini halafu wakasingizia kuwa mimi ndiye nimetoa maelekezo hayo lakini si kweli. Kama suala hilo limetokea huenda wauzaji walichanganya biashara. Nitalifuatilia kwa mkuu wa wilaya (ya Ilala) ili tujue tatizo liko wapi," alisema.

Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Edward Mpogolo, alisema hana taarifa kuhusu suala hilo na kusema kuna baadhi ya wauza magazeti si waaminifu ambao wamekuwa wakichanganya magazeti na bidhaa zingine, jambo ambalo ni ukiukwaji wa utaratibu waliowekewa.

"Baadhi yao si waaminifu wanauza magazeti lakini ukifika mchana utakuta wameweka na vitu vingine. Wanakaribisha na kuwaruhusu watu wengine kufanya biashara karibu na meza zao.

"Mfano pale Kariakoo, kuna eneo linajulikana muda mrefu kuwa ni la wauza magazeti lakini hivi sasa ukifika unakuta na watu wengine wanafanya biashara pembeni yao.

"Ninawataka wauza magazeti waje tuonane, tuzungumze wanieleze tatizo hasa liko wapi? Tuone tunalitatua vipi ili waruhusiwe wakachukue meza zao, waendelee na biashara kujipatia riziki," alisema Mpogolo.

Baada mazungumzo baina ya wauzaji wa magazeti na mkuu wa wilaya, wafanyabiashara hao waliruhusiwa kwenda kuchukua meza zao, wakisisitiziwa kulinda mazingira na kuzingatia usafi.



Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule akifungua bomba la maji kuzindua mradi wa maji wa kijiji cha Buigiri, Wilaya ya Chamwino, mkoani Dodoma juzi. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Tahadhari mvua kubwa Pwani, Zanzibar

**Na Faustine Feliciane**

MAMLAKA ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA), imewataka wananchi kuchukua tahadhari kutokana na mvua kubwa ambazo zinatarajia kunyesha kwa siku tatu kwenye mikoa ya Dar es Salaam, Tanga, Pwani na Visiwani Zanzibar. Kwa mujibu wa taarifa ya TMA iliyotolewa juzi, mvua hizo mbazo zimeanza kunyesha jana, zinatarajiwa kuendelea hadi kesho (Jumapili).

Akizungumza na gazeti hili jana, Mtaalam na Mchambuzi wa Hali ya Hewa kutoka TMA, Rose Senyagwa, alisema moja ya athari zinazotarajiwa ni makazi ya watu kuzungukwa na maji, uharibifu wa miundombinu pamoja na kukwama kwa baadhi ya shughuli za kiuchumi.

"Mifumo yetu ya hali ya hewa bado inaonyesha kuwapo kwa mvua kubwa kuanzia leo (Ijumaa) mpaka Jumapili, lakini pia bado tupo kwenye kipindi cha mvua za Masika wananchi waendelee kufuatilia taarifa za hali ya hewa tunazozitoa," alisema Senyagwa.

Alisema mamlaka husika zinapaswa kuchukua tahadhari kwenye miundombinu kutokana na mvua zinazoendelea.

"Kipindi hiki cha mvua pia, sekta ya afya na wananchi kwa ujumla wachukue tahadhari ya magonjwa ya mlipuko," alisema Senyagwa.

Februari mwaka huu, TMA ilitoa utabiri wa mvua za Masika na kuonyesha upungufu wa mvua kwa baadhi ya mikoa, lakini ikatoa angalizo kwa mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Zanzibar na baadhi ya maeneo ya Mkoa wa Morogoro kuhusu kuwapo kwa vipindi vya mvua kubwa.

Katika utabiri huo mikoa ya Tanga, Kilimanjaro, Arusha, Manyara, Kigoma na ile ya Kanda ya Ziwa ilitarajiwa kuwa na mvua za wastani hadi chini ya wastani (mvua chache).

# Mpango wa daraja la Dar - Zanzibar waja

**Na Augusta Njoji,**
DODOMA

BUNGE limeelezwa kuwa mazungumzo kuhusu ujenzi wa daraja litakalounganisha Tanzania Bara na Zanzibar yameshaanza.

Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Geofrey Kasekenya, aliyasema hayo jana bungeni jijini hapa. Alikuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Mwantumu Dau Haji.

Katika swali lake, Mbunge huyo alihoji serikali ina mpango gani wa kujenga daraja linalounganisha Tanzania Bara na Zanzibar.

Akijibu swali hilo, Kasekenya alisema mazungumzo kuhusu ujenzi wa daraja hilo yameanza na kuzihusisha Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (sekta ya ujenzi) kwa upande wa Tanzania Bara na Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kwa upande wa Zanzibar. Alibainisha kuwa mazungumzo hayo yalianza Machi 11, 2023.

Kwa mujibu wa Kasekenya, mazungumzo hayo yalianza kwa kukutana na wawekezaji Kampuni ya M/s China Overseas Engineering Group Company (COVEC) waliokuwa wameonyesha nia ya kujenga daraja hilo.

"Yatokanayo na kikao hicho bado yanafanyiwa kazi kwa pande zote mbili Tanzania Bara na Zanzibar,"alisema.



Baadhi ya wanafunzi wa Shule ya Sekondari ya Idete waliohudhuria Mahafali ya 66 ya Shule ya Sekondari ya Tabora Wavulana katika Manispaa ya Tabora, wakizungumza na Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA), Bahati Geuzye (kushoto), aliyekuwa mgeni rasmi kwenye mahafali hayo mapema wiki hii. **PICHA: MPIGAPICHA WETU.**

# Muhongo ataja mambo kusaidia Tanzania kupaa zaidi kiuchumi

**Na Gwamaka Alipipi,** DODOMA

MBUNGE wa Musoma Vijijini, Prof. Sospiter Muhongo, ametaja mambo kadhaa ambayo yataisaidia Tanzania kusonga mbele kiuchumi ikiwamo serikali kumiliki asilimia 100 sekta ya madini.

Pamoja na ushauri huo, Prof. Muhongo amesema hadi sasa sekta ya madini bado haijachangia ipasavyo katika ukuaji wa uchumi na kuondoa umaskini ambao unapaswa kukua kwa asilimia nane hadi 10. Amesema uchumi ukiwa chini ya hapo, nchi haiwezi kuondoa umaskini.

Waziri huyo wa zamani wa Nishati na Madini, akichangia mjadala wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Madini bungeni jana, alisema umaskini wa Watanzania unapaswa kupungua kutoka asimilia 20 hadi 15.

"Tangu mwaka 1961 hadi 2021 sekta ya madini inajishughulisha na utawala wa sekta ya madini ndiyo maana madini yanayochimbwa ni hayo hayo, yaani dhahabu, almasi na vito hasa tanzanite na ruby," alisema Prof. Muhongo.

Alisema uchumi wa dunia ya sasa unaongozwa na aina mbili za ubepari, kwanza ubepari wa kiserikali ambao unaendeshwa na mataifa ya magharibi, na pili ubepari binafsi ambao unafanywa na mataifa ya China, Brazil na Norway ambayo yamefanikiwa kiuchumi.

"Hivyo sekta ya madini lazima itupeleke huko ili tufanikiwe. Ni lazima tuwe na migodi inayomilikiwa na serikali kwa asilimia 100, vinginevyo hatutafanikiwa, tutadhani hizo bilioni tunazopata ni nyingi," alisema.

Prof. Muhongo alisema ili Tanzania ikue kiuchumi ni lazima Wakala wa Jiolojia Tanzania (GST) iwezeshwe ili nchi ijue ina aina gani za madini, kiasi na kujishughulisha kwenye utawala wa madini. Alisema ni jambo la ajabu kwa serikali kuweka nguvu katika Tume ya Madini badala ya GST.

Kuhusu sheria za madini, Prof. Muhogo alisema kuna sheria nyingi ambazo zinatungwa lakni kabla ya kuanza kutumika zinabadilishwa, zingine zina upungufu.

"Kwa mfano sheria hii inayosema tunapata hisa ya asilimia 16 ya umiliki kwenye kampuni za uchimbaji madini, wabunge na Watanzania mnaonisikiliza hili ni kosa kubwa tunafanya.

"Asilimia 16 hiyo tunaweza tusipate kitu kwa sababu hatuko kwenye bodi inayofanya maamuzi, kwenye vikao vya utawala hatupo, hujui unazalisha kiasi gani wala unauza kiasi gani,yaani umekaa pembeni unasubiri uletewe mauzo ya asilimia 16. Maana ya kuwa mwanahisa ni lazima ushirikiane na mwenzako katika kuwekeza na kwenye faida," alisema.

Profesa Muhongo alisema pia serikali inapaswa kuwa makini katika utoaji wa leseni za uchimbaji madini, uvumbuzi wa madini mapya

"Kwa mfano tumetoa leseni ya uchimbaji wa madini ya Platinum Group Metal, je tunajua huko wanaenda kuchimba nini? Maana yake PGM ina madini kama saba na yote yanathamani kubwa, mfano platinum, paradium, rodium.

"Madini ya rodium wakati dhabau ilipokuwa inauzwa Dola 1,850 kwa arms, rodium ilikuwa inauzwa Dola 10,300 kwa arms. Je? sisi tunajua hawa tuliowapa leseni hawatayachimba hayo?"

Kuhusu kuhifadhi dhahabu, Profe. Muhongo aliishauri serikali kuanza utaratibu wa kuhifadhi kwa sababu mataifa makubwa yanafanya hivyo. Akitoa mfano, Profesa Muhongo alisema Marekani ina akiba ya dhahabu tani 8,133, Japani tani 846 na China tani 1,948.

Akijibu baadhi ya hoja za wabunge, Waziri wa Madini, Doto Biteko alisema kwa sasa Benki Kuu ya Tanzania (BoT) ina akiba ya dhahabu tani 400.

Kuhusu hisa ya asilimia 16, alisema Tanzania ina mwakilishi katika bodi za kampuni hizo, kwamba serikali ipo makini katika kulinda mali za Watanzania.

# Afungwa jela maisha kwa kunajisi mtoto wa kufikia

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

MAHAKAMA ya Wilaya ya Kibaha mkoani Pwani, imemhukumu Dickson Chilongola (37), mkazi wa Zegereni wilayani hapa kifungo cha maisha jela, baada ya kupatikana na hatia ya kunajisi mtoto wake wa kufikia mwenye umri wa miaka 10.

Mbali na adhabu hiyo, Chilongola ameamuriwa na mahakama kuchapwa viboko 12 na kulipa fidia ya Sh. milioni mbili.

Hukumu hiyo ya kesi ya jinai namba 13/2023 ilitolewa juzi na Hakimu Mkazi Judith Lyimo wa mahakama hiyo.

Akisoma hukumu hiyo baada ya kusikiliza ushahidi wa pande zote, Hakimu Lyimo alisema amemtia hatiani mshtakiwa kwa mujibu wa kifungu 130 (1), (2) (e) na kifungu 131 (1) cha Sheria ya Kanuni ya Adhabu Sura ya 16 iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2022. Ilielezwa kuwa mshitakiwa alitenda kosa hilo mnamo Februari Mosi, 2023 majira ya usiku mtaa wa Zegereni, wilaya ya Kipolisi ya Mlandizi.

Ilielezwa kuwa mshtakiwa aliingia chumbani kwa mtoto huyo kisha kumfanyia kitendo hicho cha kikatili.

# Kampeni kisheria Mama Samia yazinduliwa

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa Majaliwa, amezindua kampeni ya kitaifa ya huduma ya msaada wa kisheria ya Mama Samia Mkoa wa Dodoma inayolenga kuboresha upatikanaji wa haki kwa watu wasiojiweza na wanaoishi kwenye mazingira magumu.

Akizungumza katika uzinduzi huo jana jijini hapa, Waziri Mkuu Majaliwa alitoa wito kwa wananchi na wadau kushirikiana na Wizara ya Katiba na Sheria katika kampeni hiyo kwa kutoa taarifa sahihi na kwa wakati.

Majaliwa alisema hatua hiyo itahamasisha utii wa sheria, kutoa elimu sahihi kwa umma, kutoa urahisi kwa waathirika wa ukatili, kutoa ushirikiano kwa vyombo vya utoaji haki, kutoshiriki matukio ya uvunjifu wa sheria na kuwalinda watoto katika maeneo yote.

"Kampeni hii inatarajia kuboresha upatikanaji wa haki kwa watu wasiojiweza,

hususan wanawake, watoto na makundi mengine yaliyo katika mazingira magumu, itachangia kuimarisha amani na utulivu, kuongeza kipato cha mtu mmoja

mmoja na kuleta utengamano wa kitaifa," alisema.

Waziri Mkuu alisema shughuli zitakazofanyika katika kampeni hiyo ni pamoja na kutoa elimu ya sheria kwa umma dhidi ya mapambano ya ukatili wa kijinsia, kutoa ushauri nasihi na huduma za kisaikolojia kwa waathirika na manusura wa ukatili wa kijinsia, kutoa elimu ya sheria kwa umma

kuhusu usimamizi wa mirathi na urithi, haki za ardhi na utatuzi wa migogoro kwa njia mbadala.

"Shughuli nyingine ni kutoa elimu ya sheria kwa umma kuhusu haki za msingi za binadamu na wajibu, kutoa huduma ya msaada wa kisheria kwenye sehemu za vizuizi - magerezani/vyuo vya mafunzo,vituo vya polisi, sehemu zenye mikusanyiko, shuleni na vyuoni," alisema.

Kadhalika, alisema shughuli zingine ni pamoja na kuwajengea uwezo katika masuala ya kisheria viongozi wa serikali za mitaa au shehia kutoa elimu ya masuala ya kisheria na haki za binadamu kupitia vyombo vya habari na mitandao ya kijamii.

"Huduma hizo za msaada wa kisheria zitatolewa bure kwa wananchi hivyo tunatoa wito kwa wananchi kutumia fulsa hii kikamilifu ili kunufaika vyema na kampeni hii, itafanyika kwa miaka mitatu kuanzia mwezi Machi, 2023 hadi Desemba, 2025 nchi nzima katika mikoa yote ya Tanzania Bara na Zanzibar,"alisema.

Alisema kwa Tanzania Bara kwa mwaka huu kampeni itafanyika katika mikoa ya Dodoma, Shinyanga, Manyara,Ruvuma, Kigoma, Morogoro, Njombe, Rukwa na Kagera na imeandaliwa na Wizara ya Katiba na sheria pamoja na Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora kwa kushirikiana na Wizara na taasisi za serikali, asasi za kiraia, wanazuoni na wadau wa maendeleo.

# TRA yasema uadilifu, uzalendo siri ufanisi ukusanyaji mapato

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA) imesema mafanikio ya ukusanyaji mapato unatokana na uadilifu na uzalendo unaoonyeshwa na wananchi.

Meneja wa Elimu kwa Mlipakodi wa TRA, Stephan Kauzeni, alibainisha hayo jana alipokuwa akizungumza kwenye mahafali ya 54 ya kidato cha sita ya Shule ya Sekondari ya Wavulana Kibaha.

Kauzeni ambaye alimwakilisha Kamishna Mkuu wa TRA, Alphayo Kidata, alisema nchi yoyote ili ifanikiwe kwenye ukusanyaji mapato, lazima walipakodi wawe na uzalendo na uadilifu.

Alisema mapato ndani ya nchi yanatumika katika kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo, hivyo kila mwananchi akitimiza wajibu wake wa kulipa kodi, mabadiliko ya kiuchumi yataonekana.

Mkuu wa Shule hiyo, George Kazi, alisema shule hiyo imeendelea kufanya vizuri kwenye matokeo ya kidato cha sita ambapo walipata daraja la kwanza na la pili.

Kazi alisema mbali na mafanikio, shuler inakabiliwa na vikwazo vikiwamo upungufu wa maji kwa kuwa wanahitaji matangi 40 ya lita 10,000 kwa ajili ya kuhifadhia maji . alisema kwa siku wanahitaji maji lita 300,000 na yanayopatikana ni chini ya lita 100,000 ambayo nayo yanapatikana kwa mgawo.

Meneja wa Idara ya Elimu ya Shirika la Elimu Kibaha (KEC), Dk. Rodetius Shemlekwa, aliishukuru TRA kwa kukusanya mapato makubwa ambapo yamesaidia elimu ya msingi bila ya malipo.

Akisoma risala kwa niaba ya wahitimu, Abdulkadir Thabit, alisema moja ya vikwazo wanavyokabiliana navyo ni uhaba wa walimu wa masomo ya sayansi, uhaba wa viti na majiko.




Diwani wa Mikocheni A Hussein Zenzel (katikati), akikata utepe kuzindua majengo mawili ya madarasa ya shule ya msingi Mikocheni A yaliyojengwa na mfadhili Ishik Foundation, jijini Dar es Salaam mapema wiki hii. Kulia ni Mkurugenzi wa Shule ya Fedha Ibrahim Yunus na (kushoto) ni Mwalimu kutoka shule ya Metis Montessori Lyecum Pinar. **PICHA: MIRAJI MSALA.**

# Waziri asema kompyuta mpakato, vishikwambi kutengenezwa nchini

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof.Adolf Mkenda amesema vishikwambi, projecta na komputa mpakato zinatarajiwa kuanza kuzalishwa nchini kuanzia mwezi ujao.

Kwa kuanza kwa mpango huo, Watanzania wamehamasishwa kununua bidhaa hizo kwenye soko la ndani badala ya kuagiza nje ya nchi. Bidhaa hizo zitaanza kuzalishwa na kampuni ya TANZTECH iliyoko jijini Arusha.

Akizungumza jana jijini hapa katika kilele cha Wiki ya Ubunifu kilichoambatana na Mashindano ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu (MAKISATU) mwaka 2023, Prof. Mkenda, alisema serikali iliipa masharti matatu kampuni hiyo ikiwamo programu ya kuanza kuwafundisha watanzania mambo ya uhandisi wa kielektroniki.

"TANZTECH wanatarajia kuanza kuzalisha vishikwambi hapa nchini na moja ya masharti ni kuunganisha vifaa mbalimbali na kutoa tablets(vishikwambi), na wanaanza mkakati wa kuzalisha hizo pads na si tu kuchukua baadhi kutoka China na kwingineko baadhi ya bidhaa zitazalishwa hapa hapa nchini," alisema. Prof. Mkenda alisema kampuni hiyo itaungana na serikali kwenye vyuo vyake vya ufundi vya vikiwamo vya mafunzo ya ufundi stadi (VETA), Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DITO, na Chuo cha Ufundi Arusha kuwasaidia wanafunzi kuingia kwenye mafunzo maalum ya mambo ya kielekroniki na uhandisi wa kielektroniki.

"Tutajitahidi kwa kadri iwezekanavyo watakapoanza uzalishaji kampuni hii na wengine wote tuache kununua vishikwambi kutoka nje, nchini zinatofautiana kwasababu ya teknolojia, tofauti ya nchi na nchi ni kwasababu ya sayansi na teknolojia na zinavyoongeza thamani na ubunifu," alisema.

Sayansi, teknolojia na ubunifu, alisema vina mchango mkubwa wa kuchagiza maendeleo ya kiuchumi na kwamba nchi mbalimbali zimefanikiwa kutokana na kuwekeza kwenye eneo hilo.

"Ibara ya 102 ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi inaahidi kuwa serikali itahakikisha inaendeleza sayansi, teknolojia na ubunifu, tunachokifanya hapa leo ni kuendeleza yale ambayo chama chenye serikali kilitoa ahadi wakati wa kuomba kura kwa wananchi, baada ya kufanya maonesho haya ya MAKISATU tunaona tunapata bidhaa zilizoibuliwa, zimebiasharishwa na ni jukumu letu kuzitangaza," alisema.

"Nchi ya Norway iliendelea kwasababu iliwekeza kwenye elimu hasa sayansi, teknolojia na ubunifu, nchi nyingi zimeendelea kwasababu ya kuwekeza kwenye sayansi na teknolojia na baadae kuziingiza teknolojia hizo sokoni, tusidhani suala hili ni dogo na wote walioanza na ubunifu walianza kwa kubezwa zamani miaka ya 50 magari ya Japan yalikuwa yakibezwa leo hii barabarani magari mengi ni ya Japan," aliongeza.

Waziri Mkenda alisema Ilani ya CCM ilipoahidi kwa wananchi kuendeleza sayansi, teknolojia na ubunifu ni jambo kubwa litakalowezesha nchi kusimama na mataifa mengine duniani bega kwa bega.

Kadhalika, alisema moja ya mambo ambayo serikali inayafanya ni pamoja na kuhimiza vijana kusoma sayansi ili kuwa kupata wataalamu wa kutosha kwenye fani za sayansi na uhandisi.

"Tulifika mahali vijana wetu wakifanya vizuri kidato cha sita wakienda Vyuo Vikuu wanatafuta kazi za kuwa Mameneja mara moja sio kwenda kufanya uhandisi, vijana walikuwa wanafanya vizuri kwenye sayansi walikuwa wanahama kwenda maeneo mengine kwa maelekezo ya Rais wetu alisema tutenge fedha tutoe ufadhili kwa wale waliofanya vizuri kwenye sayansi ili kusoma vyuo vikuu masuala ya sayansi," alisema.

Naye, Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Prof. Carolyne Nombo, alisema tangu kuanzishwa kwa MAKISATU Mwaka 2019 wabunifu na wavumbuzi wachanga wapatao 2,636 waliibuliwa na kutambuliwa na Wizara huku wengine 283 wanaendelezwa na serikali kupitia Tume ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) ili bidhaa zao ziingie sokoni.

"Serikali kupitia Buni Hub na DTB imewezesha kuanzishwa kwa kampuni changa mapya zaidi ya 94 na kutoa ajira na ajira zisizo za moja kwa moja kwa vijana zaidi ya 30,000 mchango wa kampuni hizo kwenye pato la Taifa umeanza kudhihirika ambapo hadi sasa kampuni hizo zinalipa kodi Sh.Milioni 500 kila moja kwa kila mwaka na wameajiri watu kuanzia watano hadi 30," alisema.

Nipashe
MWANGA WA JAMII




# Simba, Yanga anzeni sasa usajili wa wachezaji Afrika

**WAKATI** tuko katika wikendi nyingine ambayo mashabiki wa soka na wanamichezo wa Tanzania na nchi jirani wanaelekeza macho na masikio yao kufuatilia wawakilishi pekee wa Afrika Mashariki na Kati waliobakia katika mashindano ya kimataifa yanayoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF), Simba na Yanga wakishuka kwenye viwanja viwili tofauti, huu ni muda wa timu hizo kuanza mchakato wa usajili kuelekea msimu ujao.

Simba wao jana usiku walikuwa ugenini katika jiji la Casablanca wakivaana na wenyeji Wydad AC katika mechi ya marudiano ya hatua ya robo fainali ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, na katika mechi ya kwanza iliyofanyika kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, Wekundu wa Msimbazi walipata ushindi wa bao 1-0.

Kwa upande wa mabingwa watetezi na vinara wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga ambao walianzia ugenini kwenye hatua hiyo ya robo fainali na kupata mtaji mzuri wa mabao 2-0, kesho watawakaribisha wapinzani wao, Rivers United kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, kuanzia saa 1:00 usiku.

Yanga inashuka uwanjani ikiwa mbele, lakini inatakiwa ifahamu mechi haikumalizika kule Nigeria, inatakiwa ipambane kuhakikisha inafanya vyema na kutimiza malengo yake waliyojiwekea msimu huu.

Timu hiyo inayofundishwa na Nasreddine Nabi, raia wa Tunisia inatakiwa ifahamu kama wao walipata ushindi katika dakika 90 za kwanza kule Nigeria, hivyo wapinzani wao, Rivers United nao pia wanaweza kufanya vyema.

Katika kuhakikisha wageni hao hawafanikiwe kupindua mbeza, kila mchezaji anatakiwa kupambana kusaka matokeo chanya na hatimaye kutinga hatua ya nusu fainali ambayo imekuwa ikisubiriwa na Watanzania kwa muda mrefu, haijalishi kama tutainga hatua hiyo kupitia mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika au michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Hakuna mechi rahisi kwa timu yoyote, anayeongoza anatakiwa kupambana kulinda ushindi wake na ambaye alifungwa katika mechi ya kwanza, ataingia dimbani kwa lengo moja la kurekebisha makosa na hapo ushindani unatarajia kuonekana wakati wote.

Tunaamini Simba ambayo ilishuka dimbani jana usiku na Yanga zimeshafanya makubwa katika mashindano mbalimbali wanayoshiriki, sasa wakati zikiwa katika majukumu yake wikendi huu, tunawakumbusha kuanza maandalizi ya usajili wa wachezaji kwa ajili ya msimu ujao mapema.

Kusajili mapema wachezaji kunasaidia makocha kuandaa vikosi imara na kuacha 'kuokoteza' wachezaji wakati zikiwa zimebakia siku chache kabla ya dirisha la usajili kufungwa.

Tunakumbuka msimu uliopita Yanga ilikosa huduma ya mshambuliaji wake, Fiston Mayele, raia wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), kutokana na usajili wake kuchelewa na timu hiyo iliondolewa mapema kwenye mashindano hayo ya kimataifa huku Simba hadi leo ikiwa kwenye rada za kumwania Ceaser Manzoki, ambaye alikuwa akicheza soka la kulipwa Uganda lakini sasa tayari yuko China akiendelea kusakata kandanda la kulipwa.

Mawakala na maskauti mbalimbali wa Simba na Yanga wanatakiwa kufanya kazi yao mapema na pale watakapotakiwa kuwasilisha majina ya wachezaji wanaotakiwa kuongezwa kwa mujibu wa ripoti ya benchi la ufundi, wafanye hivyo kwa weledi kwa sababu tayari waliandaliwa.

Suala hili la usajili wa wachezaji wenye viwango vya kimataifa na wazoefu pia linaihusu Azam FC na timu nyingine zenye uwezo, kwa sababu ubora wa wachezaji ndio huzalisha ligi imara na yenye hadhi ya juu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com

## Muungwana Lazima Nilonge



# JKT Tanzania karibuni Ligi Kuu Bara iliyochangamka

Na Adam Fungamwango

**HATIMAYE** JKT Tanzania FC imerejea katika Ligi Kuu Bara baada ya kushindwa kufanya hivyo msimu uliopita, iliposhindwa kupata pointi katika mechi za mchujo.

Ilianza kwa kufungwa bao 1-0 ikiwa nyumbani kwenye Uwanja wa Meja Jenerali Isamuhyo, Dar es Salaam na kutoka sare ya goli 1-1 ugenini Mbeya, Uwanja wa Sokoine dhidi ya Prisons, ambayo nayo nusura ishuke, lakini 'play off', ikawakoa.

Wiki hii imefanikiwa kurejea katika Ligi Kuu baada ya kufikisha pointi 62 ambazo zinaweza kufikiwa na timu moja tu ya Kitayosce FC ya Tabora yenye pointi 53 kama itashinda mechi zake tatu ilizosalia.

Kitayosce inashika nafasi ya pili katika msimamo wa Ligi ya Championship, huku Pamba ya Mwanza ikishika nafasi ya tatu kwa pointi 52 na kama itashinda mechi zake tatu ilizobaki itafikisha pointi 61.

Kwa maana hiyo, rasmi JKT Tanzania ambayo ilishuka daraja msimu wa 2020/21, itacheza Ligi Kuu Bara msimu wa 2023/24.

Natoa pongezi kwa Jeshi la Kujenga Taifa kwanza uvumilivu kwani hata baada ya kushuka daraja, na kuondokewa na baadhi ya wachezaji, lakini waliwabakisha nyota wake wengine akiwamo, Edward Songo, akishikikiana na wenzake wazoefu walikuwa chachu kubwa ya kuirejesha timu hiyo na safari hii hawakutaka kikwakute kile cha msimu uliopita kucheza 'play off.'

Wakapambana na kuhakikisha wanapanda moja kwa moja.

Ilikuwa ni huzuni kubwa kwao msimu uliopita waliposhindwa kidogo tu, kwenye mechi ya marudiano Uwanja wa Sokoine, Prisons ililazimika kusubiri dakika za mwisho kusawazisha bao ambalo liliwabakisha Ligi Kuu.

Viongozi wa JKT Tanzania hawakuikatia tamaa timu yao, walisimama imara na haya ndiyo matunda yao.

Sasa timu imerejea Ligi Kuu. Na si hiyo tu, huenda Kitayosce na Pamba moja ikapanda daraja moja kwa moja, hivyo nazikaribisha kwa tahadhari kubwa.

JKT Tanzania na timu nyingine zitakazopanda daraja zikumbuke zinakuja kwenye ligi kubwa zaidi ya ile waliyotoka.

Kuna dhana Ligi ya Championship ni ngumu kuliko Ligi Kuu Tanzania Bara, lakini ukichunguza utakuta hakuna uhalisia, ila ni ligi ambayo ina vimbwanga vingi na maamuzi yenye utata, ndiyo maana ya kauli hiyo.

Ligi Kuu Tanzania Bara kwa sasa siyo ile ya mwaka 2020/21 kurudi nyuma, JKT Tanzania wenzake walijue hilo.

Wanatakiwa waje kwa heshima na adabu. Kwanza kabisa wachuje wachezaji. Kama ni vijana basi wawe wale wenye uwezo au vipaji vya ziada na kama ni wakongwe basi wale ambao wenye manufaa kwa timu, siyo walioshuka viwango na umri mkubwa.

Timu zimebadilika sana, kwani hata Ihefu ina wachezaji wenye uwezo mkubwa pamoja na nyota wa kigeni ambao wametoka kwenye klabu kubwa.

Kuna mabadiliko makubwa, hata timu za majeshi kama Prisons, Polisi Tanzania nazo kwa sasa zinasajili baadhi ya wachezaji wa kigeni na wamekuwa na msaada mkubwa katika vikosi vyao.

Timu zimekuwa zikipambana kisawasawa kiasi ni kama hakuna kibonde wa kudumu kwenye ligi hii, zikiwa zimebaki raundi nne, bado hakuna timu ambayo mpaka sasa imeshashuka daraja tofauti na msimu iliyopita, angalau moja ingekuwa imeshateremka.

Nina maana, JKT Tanzania wakati inafanya sherehe ya kupanda Ligi Kuu, iandae mikakati kabambe ya kukiboresha kikosi chake ili kukabiliana na msimu mpya ujao ambao inawezekana kabisa nao ukawa mgumu zaidi kuliko huu.

Kuna timu zinasajili wachezaji kutwaa ubingwa wa Ligi ya Mabingwa Afrika, Kombe la Shirikisho Afrika huku nyingine zikihitaji tu kucheza hatua ya makundi, baadhi kujiimarisha zaidi ili kumaliza nne bora.

Hiyo ni kengele ya kujua ni timu za aina gani ambazo itapambana nazo. Kujipanga ni muhimu ili harakati za kupanda daraja isiwe za bure na kurudi ilikotoka.

# Sababu za kushamiri biashara haramu wanyamapori zatajwa

**Na Beatrice Shayo**

MUUNGANO wa Kukabiliana na Uhalifu Mtandaoni (ACCO), umesema biashara haramu ya wanyamapori inazidi kushamiri kutokana na sababu mbalimbali, ikiwamo kufungwa kwa masoko ya biashara hiyo.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam, Mratibu wa Mtandao huo, Shubert Mwarabu, alisema uwapo wa masoko halali ya mazao ya wanyamapori zikiwamo pembe za faru na meno ya tembo, unachochea biashara haramu ya meno ya tembo.

Alisema China ambayo ilikuwa na soko kubwa la meno ya tembo, ilifunga biashara hiyo Januari Mosi, 2018 jambo ambalo mataifa mengine yalifurahia kutokana na uamuzi huo nzuri. "Inasikitika baada ya kufungwa kwa masoko halali ya mazao ya wanyamapori, kwa sasa biashara imeshamiri katika mtandao wa intaneti. Wahalifu na wanunuzi wanatumia mitandao ya intaneti kufanikisha shughuli zao za kuingiza bidhaa sokoni, kuitangaza na hata kupokea malipo kwenye mtandao wa intaneti," alisema.

Pia alisema jitihada za kupambana na biashara hiyo ni muhimu kudhibiti katika kila hatua, yaani chanzo na nchi hizo zipambane na ujangili na uharibifu mwingine wa maliasili ikiwamo misitu.

Alisema kwenye mapitio au njia zinazotumika wajitahidi kuziba mianya yote inayofanikisha kupitisha mazao ya wanyamapori, kwa sasa yamechukua sehemu kubwa kwenye mitandao ya intaneti.

Mwarabu alisema mtandao wa 'Alliance to Counter Crime online' ambao ni jumuiko la masharika, wadau, watafiti na wachunguzi dhidi ya uhalifu kwenye mtandao wa intaneti, wanaongeza jitihada kukabiliana na uhalifu huo kwa kushawishi mageuzi ya kisera na sheria zinazoendesha makampuni hayo.

Alisema kampuni zimekuwa zikichukua muda kufungia akaunti pale wanapotoa taarifa na kwamba, mabadiliko ya kisheria yatasaidia kuwajibishwa. Kadhalika, alisema kumekuwa na changamoto nyingine ya baadhi ya wananchi kutapeliwa katika mitandao ikiwamo mikopo hewa na wanaposikia fursa wajitahidi kujiridhisha kabla ya kuchukua uamuzi wowote katika mitandao.

"Kwa mfano unapopata fursa fulani usianze kuwashirikisha watu au kuiomba, hivi karibuni kulikuwa na fursa moja inaitwa 'Mama Samia Fund' ilitengenezwa linki na kutakiwa kujaza, eti Rais anatoa fund (kuwezesha) vijana, lazima kujiridhisha kabla ya kusambaza huu ulikuwa ni utapeli,"alisema Mwarabu.




Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Fatma Mwasa (kushoto), akikabidhi cheti cha shukrani kwa Mkurugenzi wa Fedha wa Kampuni ya tumbaku ya Alliance One, Festo Mwalongo, wakati wa hafla kukabidhi msaada wenye thamani ya sh. milioni 222 uliotolewa na kampuni hiyo kwa shule za msingi Kingolwira na Bungo za mjini Morogoro mapema wiki hii. Kulia ni Ofisa Taaluma wa Manispaa ya mkoa huo, Amani Mfaume. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Tani 356 za mbegu feki zateketezwa

**Na Christina Haule,**
MOROGORO

TAASISI ya Kuthibiti Ubora wa Mbegu Tanzania (TOSCI) imeteketeza tani 356 za mbegu zisizokidhi ubora katika kukabiliana na mbegu feki nchini katika kipindi cha mwaka 2020 hadi 2022.

Mkurugenzi Mkuu wa TOSCI, Dk. George Swela, alisema juzi kuwa mbegu hizo zimeteketezwa kwa sababu ya kutofikia kiwango cha uotaji na kusinyaa kupita kiasi.

Dk. Swela alizitaja aina za mbegu zilizoteketezwa mwaka 2020 kuwa na kiasi cha tani kwenye mabano kuwa ni za mboga (saba), mahindi (289), choroko (219), mpunga (moja), mtama (12) na alizeti (sita).

Alisema mwaka jana waliteketeza tani 58 za mbegu zikiwamo alizeti tani 22, mahindi tani mbili, viazi mviringo tani 29 na mtama tani tano.

Dk. Swela alisema licha ya kuteketeza mbegu hizo, tayari kesi saba zinaendelea katika mahakama mbalimbali nchini dhidi ya waliokamatwa na mbegu hizo.

Alifafanua kuwa mwaka 2021, kesi tano zilifikishwa mahakamani katika mikoa ya Ruvuma wilayani Mbinga, Songwe wilayani Momba na Mbeya katika wilaya za Mbeya na Rungwe. Pia alisema mwaka 2022, kesi mbili zilifikishwa mahakamani katika mkoa wa Mbeya.

Katika kuhakikisha mbegu feki zinadhibitiwa, alisema TOSCI hufanya ukaguzi na wanapobaini kwamba kuna mbegu iliyokwisha muda wake na bado iko kwenye maghala au dukani, huwaagiza kuziteketeza na wanaposhindwa kuziteketeza, TOSCI husimamia jambo hilo kwa kwa maslahi yao na taifa kwa ujumla.

Dk. Swela alisema wamewekeka mikakati ya kufanya ukaguzi wa kushtukiza mara kwa mara kwenye maduka na maghala ili kukomesha suala la mbegu feki au zisizo na ubora ambazo zikipandwa zinaweza kutoota au zikaota na kutoa mazao yasiyolingana na maelekezo yaliyomo kwenye nembo, hivyo kumsababishia mkulima hasara.

Mkaguzi wa Mbegu kutoka TOSCI, Fatuma Nasoro, alisema TOSCI imekuwa ikitoa elimu kwa mawakala wote wa mbegu kabla hawajaanza kufanya biashara ya mbegu ili kujua sharia, ikiwamo matumizi ya nembo ya taasisi hiyo kuonyesha mbegu imekidhi viwango.

Hivyo alitoa wito kwa wazalishaji wa mbegu kuhakikisha kwamba kabla hawajaanza biashara ya mbegu wanapata mafunzo ya uzalishaji wa mbegu ikiwemo mambo ya kuzingatia wakati wa kuzalisha mbegu.

Nasoro alisema TOSCI ni kiungo muhimu katikati ya wakulima, wafanyabiashara na wazalishaji ambayo inafanya kazi kwa uadilifu na kwa umakini ili kuhakikisha mkulima anapata mbegu iliyo bora.

## Biashara Tanzania na Malawi yazidi kupaa

**Na Joseph Mwendapole**

BIASHARA kati ya Tanzania na Malawi imeongezeka kutoka Dola milioni 85.3 mwaka 2017 hadi Dola milioni 86.7 mwaka 2022 huku serikali hizo mbili zikipania kupandisha viwango vya juu vya biashara baina ya nchi hizo.

Hayo yalisemwa jana na Katibu Mkuu Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Dk Hashil Abdalah, aliyemwakilisha Waziri wa wizara hiyo, Dk. Ashatu Kijaji, wakati wa kongamano la Biashara na Uwekezaji la MALAWI - TANZANIA lililofanyika Mzuzu, Malawi.

Kongamano hilo linashirikisha zaidi ya wafanyabiashara 300 kutoka Tanzania na Malawi ambao wanawakilisha sekta mbalimbali zikiwamo kilimo, uvuvi na uchumi wa bluu, viwanda, utalii, benki na fedha, usafiri, usafirishaji na Miundombinu, mawasiliano, madini, elimu na utalii wa matibabu.

Katibu Mkuu alisema ongezeko hilo bado halitoshi kwa kuzingatia uwezo wa rasilimali unaopatikana kati ya nchi hizo mbili.

"Kwa hiyo kuna haja ya kuendelea kusaidia sekta yetu binafsi nchini Tanzania na Malawi na kuweka mazingira mazuri ya kukua, kufanya vizuri na kufanya biashara kwa urahisi. Hii itaongeza ushindani wa Sekta ya Binafsi na matokeo yake wataweza kutumia kikamilifu fursa za kibiashara kati ya nchi zetu mbili," alisema.

Kaulimbiu ya mkutano huo ilikuwa ni "Kuimarisha Uhusiano wa Kiuchumi Baina ya Tanzania na Malawi Kupitia Biashara ya Mipaka na Uwekezaji'.

"Kama tunavyofahamu nchi zetu mbili zinafanya biashara kupitia mipakani, hivyo biashara ya mipakani ni muhimu sana kwa uchumi wetu na watu wetu kwani inachangia kwa kiasi kikubwa ajira," alisema.

Alisema biashara imekuwa moja ya nguzo dhabiti za uhusiano baina ya nchi hizo mbili kwa kukuza ukuaji wa uchumi wa mwingiliano wa kijamii na kuchochea uzalishaji.

Katibu Mkuu alisema Tanzania ina faida linganishi kutokana na eneo lake la kimkakati la kijiografia kama kitovu cha usafirishaji kwa nchi nyingine za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC).

Waziri wa Viwanda na Biashara wa Malawi, Simplex Banda, alisema Malawi na Tanzania zinashirikiana kwa njia kadhaa, kikanda na kimataifa, ikiwa ni pamoja na Tume ya Pamoja ya Kudumu ya Ushirikiano, SADC, Eneo Huru la Biashara la Bara la Afrika na Shirika la Biashara Duniani (WTO).

"Mtakubaliana nami kuwa mipango hii inaunda fursa kubwa kwa sekta zetu binafsi kunufaika nazo, na kufikia masoko yaliyopo kwa kuzingatia hili, tunapozungumzia vikwazo vya ugavi, tunatakiwa kuzingatia kuongeza tija na kuongeza thamani ili kukabiliana na changamoto za masoko ya nje," alisema.

Alisema ushirikiano wa karibu na wa kina kati ya nchi hizo mbili ni muhimu na unaweza kufuatiliwa kwa haraka kupitia utekelezaji wa mipango kama vile mfumo rahisi wa biashara, mpango wa maendeleo ya anga, dhana ya kituo kimoja cha mpaka, hitimisho la Mkataba wa Kukuza Uwekezaji na Ulinzi (IPPA).

Alisema nchini Malawi fursa za uwekezaji ni kubwa sana katika kilimo, madini, nishati, benki na masoko ya mitaji, miundombinu ya usafirishaji, utalii, habari, mawasiliano na mawasiliano (ICT), katika muktadha wa Malawi 2063.

# Katibu Mkuu awafunda watumishi TASAF

**Na Joseph Mwendapole**

WAFANYAKAZI wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) wametakiwa kufanya kazi kwa weledi na kuzingatia maadili huku wakiepuka ubaguzi wa aina yoyote katika utekelezaji wa majukumu yao.

Hayo yalisemwa jana na Katibu Mkuu Ikulu, Mululi Mahendeka, alipokuwa akifungua Mkutano wa Mwaka wa wafanyakazi hao unaofanyika kwa siku mbili katika ukumbi wa APC Bunju, Dar es Salaam.

Mahendeka alisema moja ya changamoto zinazoukabili mfuko huo ni baadhi ya wanasiasa kupotosha lengo halisi la Mfuko na kuhusisha kazi zake na itikadi za kisiasa na ukabila.

Alisema kwa kuwa wako wanasiasa kwa malengo wanayoyajua wao, wamekuwa wakieneza habari potofu kuwa kazi ya Mfuko zinahusiana na ikitadi za kisiasa, ni jukumu la wafanyakazi hao kuhakikisha wanafanya kazi kwa kufuata taratibu zilizopo na hivyo kuepuka ubaguzi wa itikadi za kisiasa, kidini na kikabila.

"TASAF ni taasisi ya Serikali na hivyo inafuata taratibu za kiserikali. Hakikisheni mnafanya kazi kwa bidi weledi na maarifa. Fuateni miongozo ya serikali ikiwamo kutunza siri za serikali," alisema. Aliitaka menejienti ya TASAF kutambua majukumu yake na kuyatekeleza kwa ukamilifu, kutembelea miradi katika mamlaka za utekelezaji, kuzungumza na walengwa na kujua changamoto zao ii iwe rahisi kuzitatua. "Fanyeni kazi sawasawa na jina la mfuko na muweke kipaumbele kwa maendeleo ya jamii," alisisitiza.

Aliwataka wafanyakazi kutunza rasilimali za taasisi zikiwamo magari, kompyuta. mifumo na kompyuta mpakato na kufanya kazi zilizopo kulingana na sera kukidhi matarajio ya Serikali kwa mfuko huo.

"Mambo ya uendeshaji wa miradi yameainishwa vizuri katika andiko la mradi lililosainiwa kati ya serikali na wadau wa maendeleo. Someni andiko la mradi kwa makini ili mjue mnachotarajiwa kufanya," alisema.

Akitoa Mwenyekiti wa Kamati ya Uongozi ya Kitaifa ya TASAF, Peter Ilomo, alisema kamati yake na menejimenti zinazingatia maelekezo hayo na wakati wa mkutano kama huo watatoa mrejesho kuhusu utekelezaji wa maelekezo.



Kamishna Msaidizi wa Polisi, Michael Deleli akiwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Vodacom Tanzania Plc, Philip Besiimire (kushoto), wakikagua injini ya moja ya magari ya kampuni hiyo alipotembelea makao makuu jijini Dar es Salaam juzi, kujifunza namna inavyozingatia masuala ya afya na usalama mahala pa kazi, ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya Siku ya Afya na Usalama Mahala pa Kazi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU.**

# Ushirikiano waipatia kampuni tuzo kimataifa

**Na Christina Haule,**
MOROGORO

USHIRIKIANO wa wafanyakazi na makandarasi wa mgodi wa Dhahabu wa Geita (GGML) ulioko mkoani Geita katika kusimamia na kuonyesha kujali afya na usalama kazini umefanikisha kuwapatia tuzo ya kimataifa ya usalama mahala pa kazi kwa mara nne mfululizo.

Meneja Mwandamizi wa Afya, Usalama, Mazingira na Mafunzo wa GGML, Dk. Kiva Mvungi, alisema hayo jana kwenye maonyesho ya Afya na Usalama Mahali pa Kazi yaliyoandaliwa na Wakala wa Afya na Usalama Mahali pa Kazi (OSHA) katika kuelekea sherehe za Siku ya Wafanyakazi (Mei Mosi).

Sikukuu hiyo inatarajiwa kuadhimishwa kitaifa mkoani hapa. Tuzo hiyo inayotolewa na kundi la kampuni za AngloGold Ashanti (AGA), GGML imeshinda mwaka 2019, 2020, 2021 na mwaka jana.

Dk. Mvungi alisema GGML wamefanya kitu tofauti na wenzao kwa kubadilisha mfumo wa mawasiliano ya kiusalama. Alisema badala ya kutoka kwa viongozi kwenda kwa wafanyakazi, waliweka utaratibu kwamba mfumo huo wa mawasiliano utoke kwa wafanyakazi kwenda kwa viongozi.

Alisema tangu wameanza kutumia mfumo huo wa kuwasikiliza zaidi wafanyakazi na makandarasi, mafanikio yamekuwa makubwa katika utendaji kazi. Alitoa mfano kuwa zaidi ya miaka 10 iliyopita hawajapoteza maisha ya mfanyakazi yeyote akiwa kazini na kwamba kwa zaidi ya miaka mitano hakuna mfanyakazi aliyeumia kiasi cha kushindwa kufika kazini.

Dk. Mvungi alisema GGML imeweka misingi thabiti ya uzalishaji kwenye usalama bila kuangalia gharama jambo ambalo baadae huzaa matunda sababu hakuna mfanyakazi anayeumia, hivyo uzalishaji unaongezeka.

"Tumefanikiwa kuweka mtambo (refuge chamber) ardhini kwenye mgodi wetu unaomwezesha mtu kuingia na kukaa humo kwa muda mrefu bila kupata madhara mara kunapotokea tatizo.

Lakini pia kwa kutumia kifaa kinaitwa 'proben radar' mwaka 2007 na 2014 tumefanikiwa kuzuia wafanyakazi wasiangukiwe na udongo na kuwaondoa eneo husika ambapo udongo ulioanguka ulimalizika kuondolewa kwa muda wa mwaka mzima," alisema Dk. Mvungi.

Awali, Mkurugenzi Mtendaji wa GGML, Terry Strong, alipongeza timu nzima ya idara ya afya, usalama na mazingira na wafanyakazi kwa kudumisha usalama wao ndani na nje ya kampuni. "Hayo ni matokeo mazuri yanayoashiria namna tulivyofanya vyema katika usalama na utendaji kazi kwa ushirikiano, najua ni kazi gani kubwa imefanywa katika kufanikisha hili na napenda kuipongeza timu ya idara ya usalama na afya wakiwamo wafanyakazi wote, makandarasi na wasimamizi ambao wamefanya kazi kwa bidii mwaka mzima kuhakikisha kila mtu anarudi nyumbani salama kufikia malengo yetu," alisema.

Mmoja wa wafanyakazi wa GGML na mwakilishi wa usalama afya na mazingira mahali pa kazi kitengo cha mazingira, Shadya Jamali, alisema ameshinda katika suala la usalama na afya mahala pa kazi kwa kujituma na kuhakikisha maeneo yote ya kazi yanakuwa salama.

Alisema ameshinda mara mbili mfululizo mwaka jana na mwaka huu kwa kuwashirikisha viongozi wa maeneo husika hasa anapokutana na vihatarishi vya kutatua muda huo kwa pamoja na kama kihatarishi ni cha kutatuliwa kwa muda mrefu, atakifuatilia hadi kitatuliwe.

# TCRA yawanoa bongo wasafirishaji vipeto

**Na Mary Geofrey**

MAMLAKA ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) Kanda ya Mashariki, imetoa elimu kwa watoa huduma za usafirishaji wa vipeto na vifurushi kwa lengo la kuwajengea uelewa na kuondoka na tatizo la matapeli na upotevu wa vitu vya watu.

Kaimu Meneja wa TCRA Kanda ya Mashariki, Ikuja Jumanne, akizungumza na waandishi wa habari wakati wa semina hiyo alisema ni elimu mwendelezo wa kampeni ya miezi minne waliyoipa jina la 'Tuma Chap Chap kwa Usalama'.

Alisema walianzisha kampeni hiyo baada ya kupokea malalamiko ya watumia huduma kupoteza mizigo na kuwapo kwa watoa huduma wasio na leseni.

Jumanne alisema TCRA inatoa leseni za usafirishaji kwa kampuni na watu binafsi wanaofanya shughuli hiyo kwa lengo la kudhibiti upotevu wa mizigo na mali za watu.

Kabla ya mwenye mzigo kutuma, alisema anapaswa kutumia mabasi ya abiria, kampuni zinazotumia magari, pikipiki na zile zinazosafirisha vipeto kupitia mtandao mwenye leseni halali ya TRA.

Alitoa wito kwa wananchi kabla ya kusafirisha kuhakikisha mtoa huduma aliyemchagua awe na leseni halali ya TRA, huduma inatolewa ofisini au eneo la biashara ndani ya jengo lenye namba ya nyumba au alama ya kudumu ya utambulisho.

Aliwataka pia kuhakikisha mtoa huduma aliyemchagua anatoa stakabadhi ya mfumo wa kielektroniki (EFD) baada ya malipo.

Watoa huduma hizo walilalamikia mawakala na watu wanaofanya kazi bila leseni ya TCRA kuwadaka wateja na kuwasafirishiria mizigo yao kwa kutumia majina ya watu au kampuni nyingine.

Meneja wa Kampuni ya Mabasi ya Galaxy, Magreth Kibiki, alisema: "TCRA leo wametupa elimu ya kutosha kuhusu jambo hili kuwa tutoe elimu kwa wateja wetu watufuate ofisini lakini pia tuwaelimishe wanaofanya kazi ya uwakala wajisajili ili kuepuka changamoto endapo mzigo wa mteja utachelewa kufika au kupotea."

Naye Ofisa Masoko na Mauzo wa Shirika la Ndege Tanzania (ATCL), Hellon Magai, alisema wanapokea malalamiko kutoka kwa wateja ikitokea mizigo imechelewa au kupotea ndipo wanabaini walitumia mawakala na sio kupitia ofisi zao.





## Wabunifu silaha waitwa COSTECH ili zitambuliwe

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

TUME ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH), imewataka wabunifu wa silaha aina ya gobole na bunduki, kuacha kuingiza bidhaa hizo sokoni kabla hazijatambulika na tume, ili kuepuka kukamatwa na serikali.

Mkurugenzi wa COSTECH, Dk. Amos Nungu, aliyasema hayo jijini hapa juzi, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kwenye maonesho ya wiki ya ubunifu yanayoendelea uwanja wa Jamhuri.

Alisema moja ya tatizo kubwa ambayo wabunifu wengi wanayo ni kutokujitokeza kuonyesha bidhaa zao ili zitambulike na kuongezwa thamani na badala yake, huingiza sokoni bila taarifa yoyote. Dk. Nungu aliwakumbusha wabunifu hao kuwa silaha huuzwa kwa utaratibu, hivyo wanapozibuni hawapaswi kuiingiza sokoni kabla ya kuziwasilisha sehemu husika kwa ajili ya kutambuliwa.

"Wasipofanya hivyo, inatuwia vigumu kutangaza bidhaa hizi, kwa sababu zitakuwa hazijatambuliwa kisheria, ninawaomba wabunifu wa bidhaa hizi waziwasilishe COSTECH kabla hawajazipeleka sokoni, "alisema.

Aliwakumbusha kwamba, faida moja wapo ya wabunifu kutambulika na COSTECH ni kuongeza thamani ya bidhaa husika na kuendelezwa kwa ajili ya kutambulika kitaifa na kimataifa, ikiwamo kuingia kwenye soko la ushindani litakalomwinua kiuchumi.

Mkurugenzi huyo alisema serikali haizuii bunifu zinazotengenezwa na wabunifu isipokuwa, inatengeneza mazingira wezeshi ambayo yanamsaidia mbunifu kuendeleza bidhaa zake, ikiwamo kutambulika na kuingia sokoni. Alisema COSTECH imesaidia wabunifu wengi ambao wamejitokeza kutambulisha bunifu zao kwa ajili ya kuongeza thamani ikiwa ni pamoja na kuziendeleza ili zitambulike kimataifa.

# Makandarasi mradi wa maji miji 28 wakumbushwa ubora

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Maji, Jumaa Aweso, amekutana na makandarasi wanaotekeleza mradi wa maji kwenye miji 28 na kuwataka wazingatie ubora.

Aweso alikutana na makandarasi hao juzi jijini hapa, kujadili masuala mbalimbali yanayohusu mradi huo wa dola milioni 500.

Mradi huo ni moja ya mradi mkubwa wa maji wa kimkakati hapa nchini na unafanikishwa na Serikali kupitia mkopo nafuu kutoka Serikali ya India kupitia Benki ya Exim ya India.

Waziri Aweso aliwataka makandarasi hao kuwa makini katika utekelezaji wa kazi hiyo muhimu ya kuwapatia watanzania huduma ya majisafi kwa kuwa, umesubiriwa kwa muda mrefu.

Alisema utekelezaji wa mradi huo ,ulianza Aprili 12, mwaka jana, baada ya serikali kukamilisha taratibu za masuala ya kodi na kulipa malipo ya awali kwa makandarasi ambao kwa sasa, wametawanyika katika maeneo yaliyo katika mpango na kazi ulioanza.

Mradi huu utanufaisha miji ya Kaliuwa, Sikonge, Urambo, Kasulu, Mpanda,Kilwa Masoko, Nanyumbu, Ifakara, Rujewa, Makambako, Njombe, Wangingombe, Chunya,Chamwino, Chemba, Singida, Manyoni, Mugumu, Geita, Kayanga, Chato, Handeni, Korogwe, Muheza, Pangani, Mafinga, Songea, Rorya / Tarime, na Makonde.




Kaimu Meneja wa Mfuko wa Barabara nchini, Mhandisi Rashid Kalimbaga, akizungumza na waandishi wa habari kuhusu masuala mbalimbali yanayohusu mfuko huo, walipotembelea banda la Bodi ya Mfuko wa Barabara katika maonyesho ya ubunifu jijini Dodoma jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TARI yabuni mashine ya kupandia pamba

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

TAASISI ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI), kituo cha Ukiriguru, imebuni mashine ya kupandia pamba huku, faida mbalimbali zikitajwa ikiwamo, kuwapunguzia gharama na kuongeza uzalishaji.

Akizungumza na Nipashe jana, kwenye wiki ya maonesho ya ubunifu jijini hapa, Ofisa Kilimo kutoka TARI Ukiriguru, Dauson Malela, alisema kuwa teknolojia hiyo itawasaidia wakulima wa pamba kutotumia jembe la mkono. "Kwa miaka mingi, wakulima wa pamba wamekuwa wakikabiliana na tatizo kubwa wakati wa upandaji, hasa katika kuzingatia kanuni za kilimo zilizopendekezwa kitaalamu, lakini pia walikuwa wakitumia fedha nyingi, tatizo ambalo linachangia kushuka kwa mavuno ya zao hilo la biashara,"alisema.

"Kilimo cha pamba kinahitaji kupandwa kwa nafasi maalumu ya angalau sentimita 60 kutoka mstari mmoja hadi mwingine na kwa sentimita 30 kutoka mmea mmoja hadi mwingine," alisema.

Ofisa huyo alisema matumizi ya jembe la mkono yanasababisha wakulima wengi kushindwa kupanda kwa kanuni za kiagronomia. "Mkulima anahitaji kuajiri wakulima tisa hadi kumi ili kupanda ekari moja, wanatumia kati ya saa nane hadi kumi. Ili kusaidia kukabiliana na tatizo hili, TARI Ukiriguru tulivumbua mashine hiyo kwa lengo la kuwezesha wakulima kulima kwa tija zaidi ili kuboresha uzalishaji wa zao hilo kwa ujumla," alisema.

Alisema awali katika safari ya uvumbuzi wa teknolojia hiyo, waliunda mashine ambayo ilikuwa ikiendeshwa na ng'ombe, ambapo wameboresha ubunifu huo kwa kutengeneza inayotumia injini.

"Tunashukuru kwa namna ambavyo Tume ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH), imekuwa sambamba katika kutusaidia kuendeleza teknolojia mbalimbali, pamoja na uvumbuzi wa mashine hii ya kupandia pamba," alisema.

Alisema mashine hiyo, inatumia lita mbili za dizeli na ina uwezo wa kupanda ekari moja ya pamba kwa kanuni husika na viwango ndani ya muda wa dakika 30 hadi saa moja.

Mtafiti Msaidizi wa kituo cha TARI Ukiriguru, Robert Cheleo, alitoa wito kwa wakulima kuchangamkia mashine hiyo ili waongeze uzalishaji.

"Tuna kila sababu ya kumshukuru, Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, kwa kuwa upande wetu kila wakati, kwa kiasi kwamba tumefanikiwa kufanya uvumbuzi wa mashine hii, na pia katika utafiti mbalimbali tunazoendela kuzifanya,"alishukuru.

Hata hivyo, alisema wanatarajia kuboresha zaidi mashine hiyo ili itumike kuanda mazao mengine kama vile maharage, mahindi na alizeti.



## Zanzibar yadhibiti malaria asilimia moja

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WIZARA ya Afya Zanzibar, imesema imefanikiwa kudhibiti ugonjwa wa Malaria ambao kwa sasa sio tishio tena na maambukizi yake yamefikia chini ya asilimia moja.

Hayo yalisemwa na Naibu Waziri wa wizara hiyo, Khamis Hassan Hafidh, wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu hali ya ugonjwa wa Malaria na mikakati inayochukuliwa kuudhibiti.

Alisema tathmini iliyofanywa mwaka jana, inaonesha kesi zilizopo za malaria ni 4,557 huku kukiwa na vifo vya watu wanne.

Alisema mafanikio hayo yamekuja baada ya kuwapo kwa mikakati mbalimbali ikienda sambamba na utoaji wa elimu kwa wananchi kuhusu matumizi ya vyandarua na kampeni za kutia dawa majumbani.

Alisema mafanikio hayo yameifanya Zanzibar kuongoza katika Nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara, zilizofanikiwa kupunguza maambukizi ya ugonjwa wa Malaria kutoka asilimia 50 hadi asilimia moja.

Katibu Mkuu Wizara ya Afya, Dk. Fatuma Mrisho, alisema mapambano dhidi ya ugonjwa huo ni endelevu na kwamba, mikakati iliyopo ni kufikia malengo ya Umoja wa Mataifa (UN) ya kuondokana moja kwa moja na vifo kwa wanawake na watoto vinavyotokana na malaria.

Meneja Mradi wa Kutokomeza Malaria, Joseph Shija, alisema wameanza kupima na kuchunguza afya za wageni wanaoingia nchini, kuona kwa kiasi gani wapo salama na maambukizi ya malaria kwa sasa.

Alisema vifaa vya uchunguzi vimewekwa katika hoteli mbalimbali za Unguja na Pemba kwa ajili ya kupata taarifa na takwimu halisi za wageni waliogunduliwa kuugua Malaria.

"Hii ndiyo mikakati yetu ya kupambana na malaria ambapo wageni wote wanaoingia nchini tutawachunguza afya zao na kuwapima kujua kwa kiasi gani wapo salama," alisema.

# Wadau wa maendeleo waitwa kusaidia matatizo sekta kilimo

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WIZARA ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo, imesema imeanza kuzifanyia kazi changamoto zinazoikabili sekta ya kilimo, na kuwaomba wadau wa maendeleo, kuisaidia ili kuongeza ufanisi zaidi.

Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Seif Shaaban Mwinyi, alisema hayo jana katika kikao kilichojumuisha watendaji wakuu wa wizara hiyo na wadau wa kilimo kutoka mashirika ya kimataifa na balozi ziliopo nchini, kilichofanyika katika ofisi za wizara hiyo, Maruhubi, Zanzibar.

Seif alisema sekta hiyo licha ya kuchangia kiasi kikubwa ya pato la taifa, bado inakabiliwa na changamoto ikiwamo ya uchache wa mabibi na mabwana shamba, vitendea kazi, kiwango kidogo cha elimu na uwezo wa watafiti jambo linalokwaza ufanisi wa sekta hiyo.

Hata hivyo, alisema wamewasilisha waraka Tume ya Utumishi Serikalini kuomba kibali cha kuajiri wa watendaji hao na kuanza kutekeleza mkakati wa kuimarisha wa mazao na mboga na matunda pamoja na kilimo hai.

"Tunatakiwa kuwa na maofisa wa kilimo (mabibi/bwana shamba) katika shehia zote 338 za Unguja na Pemba, lakini hatujazifikia shehia zote, na hata hizo tulizozifikia hatujawapatia vitendea kazi, ndio maana tumewaeleza wadau hawa waone namna ya kutusaidia," alisema.

Alisema wizara hiyo imefurahishwa na ujio wa washirika hao wa maendeleo ambao katika kikao hicho, walielezwa kwa kina kuhusu ufanisi na changamoto zinazoikabili sekta ya kilimo.

"Ujio wa hawa wenzetu umetupa matumaini ambayo yataleta msukumo katika maendeleo ya kilimo hususani kwenye uzalishaji wa mazao ya 'hotculture', utafiti na mnyororo thamani ya mazao," alisema.

Akiwasilisha taarifa ya wizara hiyo na majukumu yake, Mkurugenzi wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar (ZARI), Dk. Mohamed Dhamir Kombo, alisema sekta hiyo katika mwaka wa fedha 2022, imechangia asilimia 22.9 ya pato la taifa.

Alisema kuwa kutokana na utekelezaji wa mikakati ya kukuza kilimo, wamefanikiwa kuongeza eneo la kilimo kutoka ekari 875 za mwaka 2018 hadi ekari 1,928 mwaka huu, kutokana na kuwapo kwa maeneo ya umwagilia.

Alitaja baadhi ya changamoto zinazokabili sekta hiyo kuwa ni pamoja na mabadiliko ya tabia nchi, matumizi hafifu ya teknolojia kwenye kilimo na idadi ndogo ya maofisa ugani wenye ujuzi na uwezo wa kutosha.

Dk. Kombo aliwashukuru wadau hao kwa kuonesha dhamira ya kutaka kujua shughuli za wizara hiyo ili kuona namna watakavyoweza kusaidia kukuza uzalishaji wa mazao mbalimbali ya kilimo na mifugo nchini.

Akizungumza kwa niaba ya wadau hao, Mwenyekiti wa kundi hilo, Ofisa Programu wa Mfuko wa Kimataifa wa Maendeleo ya Kilimo (IFAD), Jaquiline Motcho, alisema kuwa ziara hiyo imelenga kujua maeneo wanayoweza kusaidia kupitia taasisi za serikali na wadau wengine wa kilimo.

Alisema kuwa kundi hilo linajumuisha mashirika 13 ya kimataifa na ofisi za Balozi zilizopo nchini, zinazotoa misaada katika sekta ya kilimo, inahusisha Wizara ya Kilimo na Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi.

Jaquiline alipongeza juhudi zinazochukuliwa na serikali za kukuza uzalishaji wa mazao ya kilimo, na kushauri mkazo kwenye uzalishaji wa mazao ya mifugo (nyama na maziwa), ili kupunguza uingizaji wa bidhaa hizo kwa kiasi kikubwa kutoka nje ya nchi.




Ofisa Uhusiano Mkuu wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa watumishi wa Umma (PSSSF), Abdul Njaidi (wa pili kushoto), akikabidhi kipeperushi cha PSSSF kwa Msimamizi Mkuu wa banda la Jeshi la Polisi, Mkaguzi Msaidizi Zuwena Mwita, wakati wa utoaji huduma kwa wanachama wa banda kwa banda kwenye maonesho ya Siku ya Kimataifa ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi katika viwanja vya Tumbaku, mjini Morogoro jana. Wa (pili kulia) ni Ofisa Matekelezo Mwandamizi wa PSSSF, Charles Mahanga. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Aga Khan kupambana na vifo mama, mtoto

**Na Mwandishi Wetu**

JUMUIYA ya Aga Khan Tanzania, imeahidi kuweka vipaumbele katika sekta ya afya ili kuhakikisha vifo vya wanawake na watoto vinatoweka kwa kutoa huduma bora.

Mwenyekiti wa Mfuko wa Taasisi ya Aga Khan duniani, Princess Zahra Aga Khan, alitoa ahadi hiyo jana wakati wa mazungumzo na Mke wa Rais wa Zanzibar, Mariyam Mwinyi, mara baada ya kufunguwa kituo cha Old Dispensary pamoja na Hospitali ya kutoa huduma za afya kwa wananchi.

Princess Zahra ambaye ni mtoto wa kiongozi wa madhehebu ya Ismailia duniani Aga Khan, alisema taasisi ya Aga Khan inayo historia kubwa kwa upande wa nchi za Afrika ya Mashariki ikiwamo Tanzania ambapo, ilifunguwa huduma za afya mwaka 1929.

Alisema mwaka 1887, Aga Khan ilijenga jengo la Old Dispensary katika eneo la Mji Mkongwe Malindi na mwaka jana ulifanyika ukarabati mkubwa wa jengo hilo.

Aliwataka wananchi wakiwamo wanawake kuzitumia huduma zinazotolewa katika kituo cha afya Aga Khan ambapo kuna vifaa vya kisasa vya kutoa huduma za afya na mikakati na kupunguza vifo vinavyotokana na kundi hilo.

Mke wa Rais alisema serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imejipanga kuhakikisha wanawake,wajawazito na watoto wanapata huduma bora za afya hadi vijijini. Alisema hivi sasa hakuna sababu ya wajawazito kujifungulia nyumbani kwa kuwa, hospitali zipo hadi vijijini na zinatoa huduma bora kwao ili kuondokana na vifo vinavyotokana na changamoto za uzazi.



**SHILOLE**
UKURASA 12

Nipashe
MWANGA WA JAMII

BT





# WAMEANZA KUPATANA?

UHASAMA kati ya wanamuziki wawili maarufu wa Bongo Fleva, Diamond Platnumz na Harmonize, unaweza kupungua kasi kutokana na kuwapo kwa dalili ya maelewano.

Wanamuziki hao waliingia katika bifu kali baada ya Harmonize kujiengua katika lebo ya WCB ambayo Diamond anaiongoza na kusababisha kila mmoja kutoa tuhuma nzito dhidi ya mwingine.

Hata hivyo, kitendo cha Diamond kukubali hadharani kwamba anajivunia kumuona Harmonize anazidi kufanya vizuri katika soko la muziki, kimewafanya baadhi ya watu kuona kuna aina fulani ya maelewano kati yao.

Siku za nyuma ilikuwa sio jambo rahisi kwa Harmonize kusema mazuri ya Harmonize, mara nyingi alinyamaza kimya au kutoa kijembe kilichoonekana kumlenga.

Diamond amesema anafurahi namna Harmonize anavyoendelea kupasua anga la muziki, jambo ambalo anajivunia.

Kauli hiyo imewashangaza wengi na kushindwa kuelewa kama pongezi hizo ni ishara ya mkono wa kirafiki ya wawili hao.

Hivi karibuni, Harmonize aliwashtua wafusi wake baada ya kutangaza ujio wa wimbo wake mpya 'Say Yes' ambao ndani yake amemshirikisha dada yake Diamond, Esma kama mwimbaji wa kiitikio.

BASI SAWA

## Esma usisikilize ya watu mwaya

ESMA Abdul, dada wa Diamond Platnumz ameonyesha kukerwa na watu mbalimbali kwenye mitandao ya kijamii kudai kuwa yupo kwenye uhusiano na msanii Harmonize.

Kupitia insta live, Esma alisema anakerwa na baadhi ya watu kwenye mtandao wa instagram wanaodai yupo kwenye uhusiano wa kimapenzi wa Harmonize wakati si kweli.



"Watu watafanya mtu uache kusapoti nyimbo za wasanii," alisema.

Maneno na minong'ono hii inakuja baada ya Harmonize kuweka wazi kuwa mwanadada huyo ndiye aliyeweka sauti kwenye ngoma yake ya ''Say Yes.'

Wabongo kama kawaida yao, eti hilo tu likatosha wao kudai kuwa huenda wana uhusiano. Lakini Esma akadai alikuwa anausapoti tu wimbo. "Watu tuache kusapoti jamani!" Akashangaa.

## Diamond amfagilia Harmonize

Wakati akifanya mahojiano nchini Ujerumani kuhusu shoo atakayoifanya, msanii Diamond Platnumz aliulizwa maswali mbalimbali, ikiwemo lebo yale ya WCB.



Akasema anajivunia namna wasanii waliotoka kwenye lebo yake wanavyofanya vizuri mpaka sasa.

Akawataja wasanii hao kubwa ni Zuchu, Mbosso, Lavalava, Rayvanny na Harmonize.

"Nafurahi kuona Harmonize anavyopasua anga kwenye soko la muziki na siyo yeye tu, hata Rayvanny, Zuchu, Mbosso na Lavalava, wote hawa ni matunda ya lebo ya WCB.

Hili liliwashangaza wengi ambao hawakutaraji kuwa msanii huyo mkubwa anaweza kumtaja mshindani wake kimuziki kwa sasa.



## WEMA, AUNT EZEKIEL USHOGA UMENOGA

Aunt Ezekiel, staa msanii wa filamu, asikwambie mtu kumbe ni rafiki mkubwa wa Wema Sepetu, ukimteta mbele yake ujue yamefika kwa mwenyewe.

Kupitia mtandao wake wa instagram, Aunt hakujizuia hisia zake kuhusu shoga 'ake huyo akiamua kumuandika kwa hisia kali jinsi anavyomkubali.

"Natamani nikwambie haya tukiwa hai bado. Wewe ni rafiki yangu mzuri sana. Siyo wa sura tu hapana. Wewe Wema ni mtu kati ya watu nikianza kukuongelea hapa, siwezi maliza natamani ujue tu, leo sina na sijawahi pata rafiki kama wewe. Kwa yote tuliyopitia Wema wewe ni zaidi. Yaani kesho nitaendelea... Nakupenda."

Mbali na kuwa wote ni wasanii wa filamu, lakini wamepitia njia moja. Ni wanamitindo waliowahi kuwania taji la ulimbwende Tanzania kwa miaka tofauti. Wema alitwaa taji la ulimbwende mwaka 1996.



## Shilole awakumbuka mama lishe

Msanii na mjasiriamali Shilole, jana aliwakumbuka akinamama wajasiriamali alipowapa msaada wa nyama kilo tano kwenye hafla iliyofanyika jana jijini Dar es Salaam.

Jumla ya mama lishe 20, walipata kiasi hicho cha nyama ya ng'ombe kutoka kwa msanii huyo wa filamu na uimbaji pia, ambaye kwa muda mrefu sasa amekuwa mjasiriamali.

"Natumai hiki kidogo, kitaenda kuwanyanyua wajasiriamali wenzangu kufukia yake mashimo madogo madogo, hii inatoka mfukoni mwangu. Na si leo tu muorodheshe majina yenu ili siku zingine mpate kilo tano tano za mchele. Tunataka akinamama kuinuana, wanawake ni taifa kubwa. Najua mna changamoto nyingine kama vile mafuta na nyinginezo," alisema Shilole huku akishangiliwa na kinamama.

Pamoja na mambo mengine baadhi ya akinamama walidai changamoto inayowakabili ni mikopo.

## MASTAA WAREMBO HALAFU WAKAJIONGEZA

**Na Adam Fungamwango**

UMAARUFU ni kitu ambacho binadamu wengi hupenda kuwa nao. Tatizo ni kwamba hauji hivi hivi. Ni lazima ufanyiwe kazi kwelikweli na muhusika ikiwa na pamoja na kujitolea bila kuchoka. Umaarufu mwingine huja tu kutokana na kipaji halisi kilichotoka kwa Mwenyezi Mungu. Hiki huwa hakifi na hakinyang'anywi na binadamu yeyote hadi pale mwenye nacho ataondoka na kipaji chake duniani.

Wakati mwingine umaarufu humfanya mtu kupata urahisi wa mahitaji yake muhimu ambayo yangemgharimu pesa, muda mwingi kuyapata, lakini kupitia ustaa wake yanarahisika.

Hapo hapo, kuna mastaa hujiongeza na kutaka kujiongezea kipato nje ya kazi yake ya kipaji.

Tumeona upande wa waigizaji wa kike, wengine wao baada ya kupata ustaa, wakaamua kujiongeza na wakautumia ustaa wao kufanya kitu kingine cha kujiongezea kipato.

**Wema Sepetu**

Ni mrembo aliyekuwa Miss Tanzania ambaye aliamua kujiingiza kwenye masuala ya uigizaji. Aliingizwa kwenye fani hii na msanii maarufu wa bongo muvi wakati huo, Steven Kanumba. Wema Sepetu mpaka sasa amecheza filamu nyingi na kuzidi kujiongezea umaarufu.

Kwa sasa anautumia umaarufu wake kujiingizia kipato kwa kazi zake mbalimbali nje ya bongo fleva na kuna wakati aliunda kampuni yake ya uigizaji, pia ni mwanamitindo.

**Shilole**

Huyu ni mrembo mwenye vipaji vingi. Ni mwigizaji na akapata umaarufu kwa kazi yake hiyo.

Lakini baadaye akageukia kwenye muziki wa kizazi kipya. Huko nako akafanya vizuri kiasi chake.

Shilole baada ya kupata umaarufu akajiongeza. Akafungua mgahawa uliokuwa maarufu tu kutokana na kumilikiwa na mtu maarufu, pia amekuwa akifanya kazi ya kusambaza vyakula sehemu yoyote anayetaka mtu apelekewe.

**Jenifer Kyaka 'Odama'**



Ni mwigizaji mrembo mwenye uwezo wa hali ya juu, si tu kuigiza, lakini hata kupambana kimaisha.

Baada ya kufanya kazi kubwa ya kutumikia filamu za kukodishwa na kulipwa ambazo kwa kiasi kikubwa ndizo zilizompatia umaarufu kwa sasa ameunda kampuni yake ambayo imekuwa ikitengeneza filamu mbalimbali.

Odama ambaye kwa sasa ndiye bosi anayechukua wasanii na kuwalipa kama alivyokuwa anafanya yeye zamani, lakini pia yeye na kampuni yake imekuwa ikiibua vipaji vipya kwa vijana wapya.

**Shamsa Ford**

Mwanadada mrembo na mwigizaji ambaye alitamba mno kwenye tasnia ya bongo movie.

Ni mmoja wa waigizaji ambao wameutumia umaarufu wao vizuri kwani amefungua duka kubwa la nguo ambalo amekuwa akilisimamia nje ya kazi yake ya uigizaji.

**Aunt Ezekiel**

Ni mwigizaji mrembo, mtoto wa mchezaji wa zamani wa Simba na timu ya taifa miaka ya '80, Taifa Stars, Ezekiel Grayson 'Jujuman'. Huyu pia ni kama Wema Sepetu, alianzia kushindana kwenye urembo, lakini hakubahatika kushinda kama mwenzake. Akaamua kujiingiza kwenye uigizaji kabla ya kuwa staa kama baba yake. Kwa kuutumia ustaa wake vizuri na kujiongeza, kwa sasa ni mfanyabiashara mzuri tu jijini Dar es Salaam.

FILAMU

## Kosa la Mama: Aibu kwa mtoto

**Na Adam Fungamwango**

FILAMU hii inaitwa 'Kosa la Mama', inaelezea baadhi ya matatizo yanayozipata familia mbalimbali ndani ya jamii.

Ndani ya familia kwenye jamii zetu kuna mambo mbalimbali ambayo yanatokea kwa uzembe au bahati mbaya, na yanaweza kusababisha matatizo makubwa au aibu mbele ya safari.

James, kijana aliyesoma vema na anafanya kazi katika kampuni fulani jijini Dar. Akapata mpenzi wake anaitwa Juddy.

Lakini baada ya muda wakabwagana na Juddy akaanza kuzusha taarifa kuwa sababu za kuachana ni kwamba jogoo la James halipandi mtungi.

Stori hiyo ikawa simulizi kazini hapo kila mmoja akiiongea kiasi kwamba ikawa ndiyo fimbo ya kumpigia. Mitaani nako yakaenea hadi yakamfikia mama yake mzazi.

Hali ikawa mbaya, kwani kila anakopita James akaanza kunyooshewa vidole. Hata hivyo mwenyewe aliamini ni jambo la kawaida na linaweza kukaa sawa.

Akakutana na binti mmoja anaitwa Sandra na akamfanyia mipango ya kuajiriwa kwenye ofisi hiyo hiyo anayofanyia kazi.

James ni mfanyakazi shupavu na mwenye kujituma kiasi kwamba alipendwa mno na bosi wake licha ya matatizo yake.

Mbali na kumfanyia mipango Sandra, lakini akaanzisha mahusiano ya kimapenzi, lakini hali ikawa ni ile ile kama ilivyotokea kwa Juddy.

Naye pia akaamua kumuacha, hivyo hali ikawa mbaya sana kwa James.

Bosi wake Kabwe alimwita ofisini na kumwambia anampenda sana kama mfanyakazi bora na hapendi kusikia maneno maneno yanasemwa juu yake, hivyo akamwambia anampa likizo ya malipo muda usiojulikana ili akatibu tatizo lake.

James la kwanza kabisa alilofanya ni kwenda kwa rafiki yake Steve ili kupata msaada wa tatizo lake ambapo sasa akakiri kuwa analo.

Ikawa kazi ya kuhangaika hospitalini na kwa waganga wa kienyeji. Mgonjwa hachagui dawa. Hivyo ndivyo ilivyokuwa.

Kila kitu kilizungumzwa kwa waganga. Wengine walidai aliwekewa tego na msichana wake wa kwanza ili asiwe na mwingine yoyote zaidi yake tu. Mmoja akadai aliangukiwa kitovu wakati akiwa mchanga na hilo ni kosa la mama yake mzazi. Na mtatuzi ni mama yake mzazi tu. Mama naye katika kuhangaika kwa waganga kumtibu mwanaye akaambiwa maneno hayo kuwa yeye ndiye atakayemtibu kijana wake kwa tatizo hilo.

Hatimaye James anapona na kuwa mwanaume kamili, kwanza anamua kumthibitishia Juddy aliyemdhihaki kuwa amepona. Alipokwenda kuhadithia Sandra naye akaja juu. Ikawa ni wivu juu ya wivu. Kati ya hao wawili, James anampenda Sandra na ndiye anayemvika pete na kumpeleka kwa wazazi huku akirejea tena rasmi ofisini baada ya kupona.





# Ayra acha wakuseme

MWIMBAJI wa muziki kutoka Nigeria, Oyinkansola Sarah Aderibigbe, maarufu kma Ayra Starr, amewajibu wale wanaomkosoa kuhusu mavazi yake kuwa wao sio wazazi wake wanaoweza kumpangia nguo za kuvaa.

Katika mahojiano ya hivi majuzi na Kiss FM, Ayra Starr amewataka kumuacha kwa sababu wao sio mchungaji wala mama yake.

Mwimbaji huyo wa 'Rush' amesema kuwa anajiamini katika uchaguzi wake wa mitindo na hua anafurahia mtindo wake wa kipekee.



## Jim amtoa chozi In Edo

MWIGIZAJI maarufu wa Nollywood, Jim Iyke, ametoa kipande cha filamu aliyofanya na Ini Edo ambacho kimesababisha kuomba radhi.

Katika uchukuaji wa picha za filamu hiyo 'Rent A Room', Jim ambaye alikuwa anaongoza alionekana kutoridhishwa na uigizaji wa Ini na kumfokea afanye maboresho, jambo lililompelekea mrembo huyo kutokwa na machozi bila kutarajia.

"Sikiliza nilikuwa nafanya mambo yangu, nikiongoza tukio hili na mmoja wa watu ninaowapenda duniani kote hakuwa akiigiza vizuri ikabidi nimzomee, nikamwambia wewe ni supastaa, duniani mimi ni kaka yako, huwezi kutaniana na mimi. Nilimfokea alikuwa analia. Lakini unajua nakupenda." Ameandika Jim

## Davido atambia mafanikio

MKALI wa Afrobeat David Adeleke, anayefahamika kama Davido, ametoa siri ya mafanikio yake ya kuwa msanii anayefuatiliwa zaidi Afrika.

Katika mahojiano ya moja kwa moja ya video kwenye mitandao ya kijamii, anahusisha umaarufu wake na utu wake wa nje, ambao umemsaidia kupata wafuasi wengi katika mitandao ya kijamii.

Davido ana wafuasi milioni 26.9 wa Instagram na wafuasi milioni 13.4 wa Twitter.

"Wizkid na Burna Boy sio watu wa kijamii kama mimi na hawachapishi mara kwa mara kama mimi. Ningechagua vichekesho vya kusisimua kama sifanyi muziki kwa sababu mimi ni kiumbe wa kuchekesha sana. " amesema





## Peter anapomkubali mwamba Wizkid

MWANAMUZIKI mashuhuri wa Nigeria, Peter Okoye amefichua kwamba aliona mapema Wizkid atakuwa maarufu katika tasnia ya muziki tangu miaka ya nyuma.


Akizungumza kwenye kipindi cha 'The 77 Podcast' cha DW akiwa na kaka yake Paul, alisema kwamba hakuwahi kumdharau Wizkid wakati wa siku zake za mwanzo na alikuwa na matumaini makubwa kwake. Amewakosoa waandishi wa habari ambao walimkataa Wizkid kama msanii anayekuja kwa kasi kipindi hicho, na kusema kwa ujasiri Wizkid hatimaye amechukua tasnia hiyo.

## Mwigizaji afariki akijibadilisha umbo

MWIGIZAJI Saint Von Colucci (22) kutoka Canada, amefariki dunia wakati akifanyiwa upasuaji wa kujibadilisha mwonekano awe kama Jimin, mwimbaji kutoka kundi maarufu la K-pop.

Muigizaji huyo alitumia dola 220,000, sawa na shilingi milioni 517, katika juhudi za kufanya upasuaji huo.

Hata hivyo, Von Colucci alipata matatizo kutokana na upasuaji huo na alifariki katika hospitali moja nchini Korea Kusini asubuhi ya Jumapili, Aprili 23, kama ilivyoripotiwa na AceShowBiz.





## HABARI KASKAZINI



Mkuu wa Wilaya ya Mwanga, Abdalah Mwaipaya akizungumza baada ya kuweka jiwe la msingi la ujenzi wa tangi la maji lenye ujazo wa lita 500000, litakalosaidia wananchi zaidi ya 14000 katika Mamlaka ya mji mdogo wa Mkuu na kijiji cha Ikuini wilayani Rombo, mkoani Kilimanjaro juzi. **PICHA: MARY MOSHA**

# Paroko aonya waume kuingilia wake zao kinyume cha maumbile

**Na Allan Isack,** ARUSHA

PAROKO wa Parokia ya Mtakatifu Moyo Safi wa Jimbo Kuu Katoliki la Arusha, Festus Mangwangi, amekemea na kuwaonya baadhi ya wanaume wenye tabia ya kuwaingilia wake zao kinyume na maumbile, kuwa dhambi hiyo haitawaacha salama.

Paroko Mangwangi, alisema hayo jana wakati akiendesha ibada kwa waumini 51 waliofunga ndoa za masuria katika kanisa hilo lililoko Ungalimitedi jijini hapa.

"Wanaowaingilia wake zao kinyume na maumbile dhambi hii itawatafuna na yatawakuta kama yaliyotokea Sodoma na Gomora, kwa kuwa kufanya hivyo ni chukizo mbele za Mungu,"alionya.

Paroko huyo amewasihi Watanzania kupiga vita ndoa za jinsia moja na ukatili wa kijinsia kwa watoto na wanawake, kwa kuwa huo siyo utamaduni kwa jamii za Kitanzania.

"Inakuaje mwanaume unaishi na mwanamume mwenzako au mwanamke uishi na mwanamke ambaye ni jinsia yako,halafu mnapambana kwa nguvu kudai haki, jambo hili ni baya sana na halikubaliki, lazima kila mmoja kwa nafasi yake kuchukua hatua ikiwamo kupiga vita.

"Wimbi la ndoa za jinsia moja linakua kwa kasi, tusipochukua hatua za kupambana na jambo hili,hapo mbeleni tunaweza kuja kuwa na viongozi wa dini,viongozi wa serikali na vyama mashoga," alidai.

Pia, amewataka wazazi na walezi, kuwafundisha watoto maadili mema na wanapoona wanajifunza vitu ambavyo ni kinyume utamaduni Kitanzania, wachukue hatua haraka iwezekanavyo ikiwamo kukemea na kuwaonya.

Kadhalika aliwakumbusha wana ndoa hao kuishi kwenye sakramenti ya Bwana ikiwamo, kushiriki shughuli za kanisa, pamoja na kutokujihusisha na mambo kinyume na imani.

"Mkitoka hapa mkaishi maisha amani na upendo sambamba na kushirikiana kwenye kila jambo kwa kuwa mmefunga ndoa, majaribu mengi yatajitokeza, hivyo mnatakiwa msimame imara.

"Mungu anataka watu waishi pamoja wakiwa tayari wameshafunga ndoa na wapate watoto wakiwa ndani ya ndoa, kwa kuwa watoto wanaozaliwa nje ya ndoa ni wa zinaa, hivyo fungeni ndoa ili mkaishi maisha matakatifu ambayo yatampendeza Mungu," alisema.

# RIVACU yaomba kurejeshewa mashamba yao yaliyotaifishwa

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

CHAMA Kikuu cha Ushirika Mkoa wa Manyara (Rift Valley Cooperative Union-RIVACU), kimemwomba Mkuu wa Mkoa huo, Makongoro Nyerere, kuwasaidia kufikisha ombi lao kwa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, la kutaka kurejeshewa mashamba yao ambayo yalitaifishwa na serikali.

Mwenyekiti wa RIVACU, Yuda Sulle, aliwasilisha ombi hilo rasmi kwa Mkuu wa Mkoa wakati wa Mkutano Mkuu wa 33 wa chama hicho.

Akizungumza katika mkutano huo, Sulle alisema pia wana mashamba ambayo yamekuwa kwenye mgogoro wa muda mrefu na Kanisa Katoliki, likiwamo shamba la vipini lililoko Wilaya ya Karatu na la Wilaya ya Ngorongoro.

Alisema shamba la vipini, lina ukubwa wa ekari 713, Irgobawe lenye ekari 353 na la Mwada lililoko Wilaya ya Babati lina ukubwa wa ekari 270.

"Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa, tunaomba utufikishie kilio chetu kwa Rais Samia, ambaye ndio mwenye dhamana ya kufuta mashamba ili atusaidie turudishiwe mashamba yetu," alisema Sulle.

Mwenyekiti huyo alivitaja vikwazo wanavyokabiliana navyo kwa sasa, kuwa ni kesi za mashamba, ugumu wa upatikanaji wa mikopo kutoka taasisi za fedha, vyama kutolipa michango yao kwa wakati, mabadiliko ya tabianchi na mfumo wa stakabadhi ghalani kupigwa vita na wafanyabiashara kwa maslahi yao binafsi.

Kuhusu shamba la Mwada ambalo kulikuwa kujengwe uwanja wa ndege, Mkuu wa Mkoa huo, amewaruhusu wananchi hao kuendelea kulitumia kwa shughuli za kilimo mpaka hapo serikali itakapolihitaji kwa matumizi yaliyopangwa.

Aidha, Makongoro aliwataka kusimamia vizuri vyama vyao na wapate viongozi bora kwa kuwa ushirika ni maisha na ni utajiri.

Pia aliwaagiza maofisa ushirika kutoka ofisi yake kushirikiana na RIVACU ili kuhamasisha mfumo wa stakabadhi ghalani ili kusaidia wakulima kupata faida.

# EU yapongezwa kuleta mradi kulinda maliasili

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

SERIKALI imeushukuru Umoja wa Ulaya (EU), kupitia Sekretarieti ya Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC), kwa kuleta nchini mradi wa kuimarisha uhifadhi wa rasilimali za maliasili na utunzaji mazingira ya uhifadhi ili kuzilinda.

Akizungumza jana Jijini hapa, Mkurugenzi Msaidizi Idara ya Wanyamapori kutoka Wizara ya Maliasili na Utalii, Fortunata Msofe, alisema mradi huo ni muhimu kwa kuimarisha uhifadhi kwenye nchi hizo.

Msofe alikuwa akizungumza na washiriki wa warsha ya siku mbili kutoka nchi za Msumbiji, Malawi, Zambia na Tanzania, ambao wamekutana kujadili suala la ushirikishwaji wa rasilimali za maliasili na namna ya kufanya jitihada za kupambana na taka ngumu hasa maeneo ya uhifadhi.

"Uhifadhi unapoimarika unawezesha wanyamapori kuwa salama. Huu ni mradi wenye manufaa makubwa kwa nchi nne unakotekelezwa. Sehemu ya mradi huu ni kuhakikisha tunakuwa na mbinu za kupunguza uchafu, kwa sababu maeneo mengi ya uhifadhi kuna shughuli mbalimbali zinazosababisha ongezeko la uzalishaji uchafu hasa mifuko ya plastiki," alisema.

Pia alisema utasaidia kupunguza ukusanyaji uchafu na mazingira yatakuwa safi na salama kwa wanyamapori.

Kuhusu usafi wa mazingira, alisema watatumia mbinu za Chuo cha Kimataifa cha Usimamizi wa Wanyamapori (MWEKA), kupitia utafiti wao kwenye maeneo ya uhifadhi na kushirikisha wananchi katika kuhakikisha uchafu unaozalishwa utumike kwenye mnyororo mwingine.

Mhadhiri wa Chuo hicho cha MWEKA, Dk. Kwaslema Malle, alisema mradi huo wa kujenga uwezo wa utafiti na ubunifu katika masuala ya maliasili na mazingira, utasaidia kuwa na matumizi sahihi ya mazingira ya uhifadhi.

Pia alisema utajikita kwenye utafiti na mafunzo kwa vyuo vinavyohusika na utafiti wa vyuo vya kati na taasisi za utafiti zinazojihusisha na mazingira pamoja na rasilimali za asili.

Alisema wanaamini mradi huo, utasaidia kuboresha mitaala ya ufundishaji na kuboresha sera zinazotumika katika kusimamia mazingira na rasilimali za asili.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Muungano wa Jumuiya za Hifadhi za Wanyamapori Tanzania, Mohamed Kamuna, alisema wamepata heshima kubwa kuwa sehemu ya mradi huo unaofadhiliwa na SADC.

## TULIKOTOKA, TULIPO & TUNAKOKWENDA...

# Ugaidi ulikaribisha marufuku kuzuru, Uwanja wa Ndege wikiendi, sikukuuu

**Na Adam Fungamwango**




SHIRIKA la Ndege Tanzania, linawatangazia kuwa ndege namba 5 H, inawasili kutoka Arusha...” Sauti hiyo nyororo ya kike ambayo inakupa picha tu kuwa anayezungumza lazima atakuwa msichana mrembo, inarudia tena maneno hayo kwa lugha ya kiingereza.

Kabla ya maneno hayo kunakuwa na mlio kama kengele hivi, ndipo maneno hayo yanatamkwa.

Na kweli mnaangalia mnaona ndege iko hewani inatua taratibu kwa madaha hivi, kabla ya matairi yake kugusa ardhi.

Hayo ndiyo yalikuwa maisha ya Watanzania kwenye miaka ya 1970, hadi katikati ya miaka ya 1990 hivi.

Nazungumzia kuzuru au kwenda Uwanja wa Ndege Dar es Salaam, wakati huo kabla haujaitwa wa Julius Nyerere.

Napoandika makala hii kuna watu wanaweza kuona kama ndoto, au aina uhalisia wowote hasa vijana wa kizazi cha sasa na ambao hawajawahi kusomuliwa aa kuliona hilo.

Kwenye miaka hiyo, watoto, vijana na watu wazima waliokuwa wakiishi jijini Dar es Salaam, au hata wale waliotoka mikoani kuja Dar kwa likizo, kusalimia ndugu au kikazi, walikuwa wakipata fursa ya kwenda kwenye Uwanja wa Ndege ili kuziangalia tu zilivyopaki pale uwanjani, zinavyotua na kupaa.

Nadhani asilimia 90 ya watoto wa zamani waliozaliwa au kukulia Dar es Salaam miaka hiyo watakuwa wameshazuru mara kadhaa Uwanja wa Ndege.

Kwanza kabisa ulikuwa ni kama mtoko wa familia. Ni kama baba au mama anavyowachukua watoto wake na kuwapeleka mbuga za wanyama, ‘beach’, au sehemu nyingine yoyote ya michezo ambayo watafurahi.

Moja ya sehemu hizo ilikuwa ni Uwanja wa Ndege Dar es Salaam. Hasa siku za wikiendi au sikukuu watu walijazana uwanjani kuangalia ndege zinavyotua na kupaa

Na hii ndiyo ilikuwa ndiyo raha yenyewe uwanjani hapo. Siku ambayo huoni ndege ikipaa au kutua watu hawafurahi, hasa watoto.




Siku ya bahati zikiwepo ndege kubwa zinapaa au kutua inakuwa ni ya furaha sana kwa watu wote na zikishaondoka watu pia wanaondoka.

Kuna watoto watundu nao waliokuwa wakiishi maeneo ambayo si mbali na uwanja, wakishatoka shule, wanakwenda.

Wakati wa likizo ndiyo kabisa, baadhi ya watoto wanashinda huko huko.

Pia ilikuwa huwezi kufika bila kukuta vijana na watu wazima. Kumbuka kuwa hapa nauzungumzia ule uwanja wa ndege wa mwanzo kabisa ambao kwa sasa umekuwa kama ni uwanja maalum kwa kushukia viongozi au kuna tukio maalum. Ni ule wenye jengo lenye rangi jekundu ambalo ukitoka mjini uwanja wa mwisho kabisa. Ule ndiyo ulikuwa uwanja mkuu zamani.

Kule juu kulikuwa na mabenchi mengi, maalum kwa watu au wananchi kwenda kuangalia. Na hakukua na matatizo yoyote, tena bure bila kiingilio.

Baada ya kukamilika uwanja mwingine ambao unajulikana kama terminal 1, kule juu nako walifanya kama ule mwingine na watu wakawa wanamiminika kwenda kuangalia ndege kama kawaida.

Dalili za marufuku zilianza katikati ya miaka ya 1990, hasa baada ya kushamiri kwa mambo ya ugaidi. Kwanza kabisa mambo yalianza kwenye ule uwanja ambao wakati huo uliitwa mpya, watu wakaanza kusachiwa kabla ya kupanda ngazi kwenda juu kuangalia.

Kila mtu mtoto na mkubwa alisachiwa kama vile inavyokuwa unapoingia kwenye sehemu zozote nyeti.

Baadaye ikawa hakuna namna tena, wakazuia kabisa.

Terminal 2- na 3 zilijengwa miaka mingi baada ya zuio, na ndiyo maana kama utakuwa mdadisi utagundua utofauti wa ujengaji kati ya kile cha mwanzo kabisa ambacho kwa sasa ni maalum tu hakitumiki kwa ndege za raia, na kile kilichojengwa badala yake.

Aina ya ujenzi wake unaona kabisa hauruhusu watu wa kawaida kufika kwa urahisi, tofauti na hivi vya sasa vilivyojengwa baada ya ugaidi ambavyo mbali na kujengwa kisasa zaidi, lakini kuna ugumu wa kuufikia kama huhusiki kusindikiza mgeni, kupokea au kusafiri.




**Tuma meseji 0716 350534.**

HABARI KITAIFA

# Mapya yaibuka mahakamani sakata la makanisa Kenya

**NAIROBI, Kenya**

MAOFISA wa upelelezi nchini Kenya wameiambia mahakama nchini humo kuwa wana ushahidi wa kuaminika kwamba baadhi ya watu waliofariki katika kanisa la Odero walizikwa huko Shakahola katika eneo linalomilikiwa na kiongozi wa madhehebu ya Kilifi, Paul Mackenzie.

Kwa mujibu wa vyombo vya habari vya Kenya, Mhubiri mwenye utata Ezekiel Odero na kiongozi wa madhehebu ya Kilifi Mackenzie ni watu wanaofahamiana, taarifa iliyowasilishwa katika mahakama ya Shanzu jana.

Nation iliripoti kuwa maofisa wa upelelezi waligundua uwepo wa uhusiano wa karibu kati ya Odero wa Kanisa la New Life lenye makao yake Mavueni na Mackenzie ambaye anadaiwa kuwashawishi wafuasi wake kufunga mpaka kufa ili kukutana na Yesu. Inaelezwa kuwa wafuasi zaidi ya 100 wanadaiwa kupoteza maisha kwa ibada hiyo ya 'kufunga mpaka kufa'. Maofisa wa upelelezi pia walisema wamefuatilia miamala ya fedha na kubaini kuwepo kwa muamala wa Sh. milioni tatu katika miamala ya kifedha kati ya Odero na Mackenzie inayotajwa ni kwa ajili ya kuuzia kituo cha TV.

Odero alikiri kununua kituo hicho cha TV kutoka kwa Mackenzie lakini akasema biashara hiyo haipaswi kuhusishwa na vifo vya Shakahola.

Pia Odero anatuhumiwa kwa mauaji, kusaidia watu kujiua, utekaji nyara, itikadi kali, mauaji ya halaiki, uhalifu dhidi ya ubinadamu, ukatili wa watoto, ulaghai, utakatishaji fedha na kusaidia uhalifu, mahakama kesi ikisikilizwa Mahakamani.

**BBC**

## Kamanda mkuu Jeshi la EAC DRC ajiuzulu

**KINSHASA,** DRC

KAMANDA Mkuu wa jeshi la Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) Meja Generali Jeff Nyagah amejiuzulu nafasi hiyo na kurudi Nairobi nchini Kenya.

Inaelezwa kuwa Nyagah aliandika barua kwa uongozi mkuu wa jumuiya ya Afrika mashariki akitoa sababu zake za kujiuzulu, akieleza kwamba usalama wake umekuwa katika hali ya hatari nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) na kuathiri utendajikazi wake.

Alisema kwamba kuna mikakati inayoonekana baina ya kuathiri utendakazi wa jeshi la EAC licha ya kutokutaja wahusika, na kwamba barua hiyo imeandikwa moja kwa moja kwa katibu mkuu wa jumuiya hiyo.

Pia ilielezwa kuwa aliripoti kwa katibu mkuu kwamba kumekuwepo juhudi za kuchunguza mahali alipokuwa akiishi, ikiwemo kuweka kamera za siri kumchunguza, pamoja na ndege zisizokuwa na rubani kupaa sehemu anayoishi na kufuatilia oparesheni za kikosi chake cha jeshi.

Alibainisha kwamba juhudi hizo zilianza mapema Januari mwaka huu. Vile vile, Meja Generali Nyagah alisema kwamba kuna kampeni katika vyombo vya habari dhidi ya kikosi cha jeshi la EAC, zinazodai kuwa wanajeshi hao wanashirikiana na waasi wa M23 badala ya kuwapiga na kuwamaliza nguvu.

Barua ya Nyagah amedai kwamba serikali ya DRC, imekuwa ikitaka uongozi wa jeshi la EAC uwe wa kupokezana, kinyume na ilivyo katika makubaliano ya jumuiya ya Afrika mashariki.

Alisema kwamba EAC inaonekana kutompa msaada anaohitaji, ikiwemo kufunga ukurasa wa facebook wa jeshi hilo, akidai kwamba ni mojawapo ya juhudi zisizo za moja kwa moja kufadhaisha kazi ya jeshi la EAC.

Serikali ya DRC ilikosa kutoa pesa kwa ajili ya kufanikisha kazi ya jeshi la EAC, ikiwemo kulipia gharama za makao makuu ya jeshi hilo, umeme, na mishahara kwa wafanyakazi wa kiraia wanaofanya kazi katika makao makuu ya jeshi hilo, kama ilivyo katika makubaliano ya jumuiya ya Afrika Mashariki.

Meja Generali Nyagah, pia anasisitiza kwamba hana uhakika na usalama wake na kwa hivyo hawezi kuendelea kuongoza jeshi la EAC nchiniDRC.

**VOA**





Maofisa wa zimamoto wakipambana kuzima moto katika nyumba moja nchini Ukraine baada ya makombora ya Russia kuishambulia nchi hiyo usiku wa kuamkia jana. **PICHA: RFI.**

## Russia yaua 19 Ukraine mashambulio miezi 2

**MOSCOW,** RUSSIA

RUSSIA imerusha makombora katika miji kote nchini Ukraine na kuua takriban watu 19 katika mashambulio makubwa ya kwanza ya anga katika kipindi cha karibu miezi miwili.

Inaelezwa kuwa Russia iliishambulia kwa makombora Ukraine usiku wa kuamkia jana, na kwamba mashambulizi hayo ya awali yalitekelezwa wakati Kyiv inajiandaa kufanya mashambulizi ya kujaribu kulirejesha tena eneo lililokaliwa na Russia.

Gavana wa mkoa Ihor Taburets, alisema katika jiji la kati la Uman, wazima moto walipambana na moto mkali katika jengo la makazi ambalo lilikuwa limeshambuliwa kwenye ghorofa ya juu, na kwamba takriban watu 10 waliuawa, wakiwemo watoto wawili, na tisa walipelekwa hospitalini.

Aidha, wakati hayo yanaendelea Rais wa Russia Vladimir Putin, alitia saini amri inayowapa watu wanaoishi katika sehemu za Ukraine chini

ya udhibiti wa Moscow njia ya kupata uraia wa taifa lake, na kwamba wale wanaokataa wanakabiliwa na uwezekano wa kufukuzwa.

Amri hiyo inaenea hadi maeneo manne ya Ukraine ambayo Russia imedai kuwa chini yake na inadhibiti kwa kiasi maeneo kama Donetsk, Luhansk, Kherson na Zaporizhzhia.

Kyiv ilisema itachukua tena maeneo yote manne, huku ikiishutumu.

Moscow kwa kujaribu kuwashawishi raia wake kukubali uraia wa Russia. Inaelezwa kuwa amri mpya inaweka njia ambazo raia wa Ukraine au wale walio na hati za kusafiria zilizotolewa na jamhuri zilizojitenga zinazoungwa mkono na Russia, na wanaoishi katika mikoa minne, wanaweza kuanza mchakato wa kuwa raia wa Russia au kuhalalisha hali yao kwa mamlaka ya taifa hilo.

Lakini pia inasema kuwa yeyote ambaye hatachukua hatua hiyo ifikapo Julai mosi 2024 atachukuliwa kuwa raia wa kigeni, jambo ambalo litawaacha katika hatari ya kufukuzwa kutoka eneo ambalo Russia inaona ni lake.

Agizo hilo pia linaruhusu mamlaka kuwatimua watu kutoka maeneo hayo manne ikiwa wanachukuliwa kuwa tishio kwa usalama wa taifa au kushiriki katika kile ambacho amri hiyo inarejelea kuwa maandamano yasiyoidhinishwa.

## RSF Sudan yashambulia ndege ya Uturuki

**KHARTOUM,** SUDAN

KIKOSI cha Msaada wa Haraka cha Sudan (RSF) kimeshambulia kwa risasi ndege ya Uturuki ilipokuwa ikitua kwenye uwanja wa ndege wa

Wadi Seyidna nje ya mji mkuu wa Khartoum. Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na jeshi la Sudan, RSF ilishambulia ndege hiyo ya Uturuki jana na kuharibu mfumo wake wa mafuta. Inaelezwa kuwa mamia wamefariki dunia na maelfu ya watu

wamekimbia katika wiki mbili za vita kati ya wapinzani wa kijeshi katika taifa hilo.

Pande hizo mbili zilikubaliana siku ya Alhamisi kurefusha muda wa usitishaji mapigano kwa saa 72 ili kuruhusu misaada ya kibinadamu, lakini mapigano yalianza tena katika baadhi ya maeneo ya mji mkuu Khartoum jana.

**VOA**

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**FOMU MIRATHI - 2**
**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya KAHAMA**
**Kituo cha KAHAMA Mkoa SHINYANGA**
**Usimamizi wa Mirathi Na. 4/2009**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU MARY MULUNGWANA WA TABORA ROAD KAHAMA**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOTOLEWA NA BAHATI MASANJA**
**TANGAZO**
**(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za usimamizi wa mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 25 Mwezi May Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**
Endapo kama yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
Imetolewa leo tarehe 21 Mwezi wa 4 Mwaka 2023.

## KUPOTELEWA NA KADI YA GREDA

SALUM MOTOR TRANSPORT LTD ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GREDA AINA 140H YENYE NAMBA ZA USAJILI T 284 ANZ. KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI KAH/TR /RB/278/2023

**IN THE DISTRICT MAGISTRATE COURT OF DODOMA AT DODOMA**
**Probate and Administration Cause NO. 38 of 2023**
**In the matter of the estate of the late**
**SHIDA EZEKIEL MAFURU**
**And**
**In the matter of application for letters of administration by**
**EDA EZEKIEL MAFURU AND ISAAC EZEKIEL MAFURU**
**GENERAL CITATION**
**(Rule 75of Probate Rules Rule Gn. 369 of 1963)**

**ALL PERSONS** Claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Admirations made to the above named petitioners.
Objections to the grant should be filed on or before the 09th Day of MAY, 2023.
Dated at Dodoma this 19th day of APRIL, 2023

1ST ........ PETITIONER

2ND ........ PETITIONER

PRINCIPAL/SENIOR/RESIDENT MAGISTRATE

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA, MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Makahaka ya Mwanzo ya Wilaya ya Missenyi**
**Kituo cha Kanyigo Mkoa wa Kagera**
**Usimamizi wa Mirathi Na. 05/2023**
**Katika Shauri la Mirathi ya Marehemu**
**CHRISTOPHER KATO BYASHALIRA wa Kigarama.**
**Katika Shauri la Maombi ya Kumteua Msimamizi yaliyoletwa na**
**KAIGARULA CHRISTOPHER BYASHALIRA.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 20 Mwezi 05 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Zingatia: Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa marehemu anaweza kuleta mahakamani kukaguliwa.
Imetolewa leo Tarehe 19 Mwezi 04 Mwaka 2023

**HAKIMU**

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA DODOMA**
**LILILOKO DODOMA**
**MAOMBI NA. 258 YA 2022**
**ROBERT NGOSI SECHEMI (as administrator the late Ngosi Sechema Jacka) ............MDAI**
**VERSUS**
**JOHN NGOSI ............MDAIWA 1**
**LOTWA SEMBELI...............MDAIWA 2**

**KWA:**
**LOTWA SEMBELI**

**POPOTE ULIPO.**
**YAH: KUITWA SHAURINI**
Kwa kuwa muombaji ameleta maombi yake ambayo maelezo yake yameelezwa katika Nakala ya maombi ambayo inapatikana katika Baraza hili.
Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria katika Baraza hili wewe binafsi, Wakili au Mwakilishi yeyote ambaye anaruhusiwa kisheria tarehe 02.05. 2023 saa 3:00 asubuhi. Kwa mujibu wa maombi hayo unatakiwa kuleta utetezi wako kwa maandishi.
ANGALIZO: kama haukuhudhuria tarehe iliyotajwa hapo juu, Baraza likithibitisha kuwa umepokea hati ya Wito, Baraza linaweza kutoa Hukumu dhidi yako.
Hati hii imetolewa kwa amri yangu na Lakiri /Muhuri wa Baraza hili leo tarehe 21 ya mwezi wa APRILI, 2023.

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

RICHARD ALPHONCE MADUHU anatangaza kupotelewa na kadi ya Gari yenye namba za usajili T660DGY aina ya SUZUKI CARRY, Rangi Nyeupe na yenye Engine No. F6A6411220 na Chasis No. DD51T439120.Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu kwa kumbukumbu namba DOD/DOD/RB/143989/2023

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

Ndugu **JOHANSENI JOAS NDYAMUKAMA** anatangaza kupotelewa na kadi yake ya gari aina ya Toyota Hiace lenye namba za usajili **T 718 AHN.** Ametoa taarifa polisi na kupewa namba **KAG/MUL/RB/146432/2023.** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi au apige simu namba **0754511515**

**FOMU MIRATHI - 2**
**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya TEMEKE**
**Kituo cha JUMUISHI Mkoa DAR ES SALAAM**
**Usimamizi wa Mirathi Na. 4/2009**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU MOHAMED SEIF KAWEMBA WA MAGOMENI**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOTOLEWA NA MAHMOUD BAKARI MANGWANGI**
**TANGAZO**
**(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za usimamizi wa mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 22 Mwezi 05 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Zingatia;
Endapo kama yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
Imetolewa leo tarehe 28 Mwezi wa 04 Mwaka 2023.

HAKIMU

**IN THE DISTRICT LAND AND HOUSING TRIBUNAL FOR KAHAMA AT KAHAMA**
**APPLICATION No. 04 of 2023**
**ERNEST MUSA MAZIGWA......APPLICANT/APPELLANT**
**VERSUS**
**KASHINDYE IGOGO.........RESPONDENT**
**SUMMONS/NOTICE**

**TO: KASHINDYE IGOGO**
**TAKE** notice that, the above matter is coming for mention on 05 of 05...2023 before Hon. LEKAMOI, P.L.S Chairman of the Tribunal. You are hereby commanded to appear at 3:00 am/pm when the case will be mentioned/heard.
Given under my HAND and the SEAL of this tribunal this 20 day of 04, 2023.

**CHAIRMAN**

**SHERIA YA UMILIKI WA ARDHI YA MWAKA 1999**
**KUPOTEA KWA BARUA YA TOLEO YA KUMILIKI ARDHI**
**BARUA YA TOLEO YENYE KUMB Na. KTA/2440**
**MMILIKI ALIYEANDIKISHWA: ZAINABU ABDALLAH – S.L.P 532, KOROGWE**
**ARDHI: KIWANJA NAMBA 37 KITALU 'J' NEW KOROGWE TOWNSHIP**
**HALMASHAURI YA MJI KOROGWE**
**MWOMBAJI: OMARI JUMA SHEKIONDO – S.L.P 532, KOROGWE**

Taarifa inatolewa kwamba BARUA YA TOLEO YA KUMILIKI ARDHI iliyotajwa hapo juu imepotea na inakusudia kutoa NAKALA HALISI YA BARUA YA TOLEO YA KUMILIKI ARDHI iwapo hakuna pingamizi litakalotolewa kwa muda wa mwezi mmoja (1) tangu tarehe ya taarifa ilipotangazwa katika gazeti.
BARUA HALISI YA TOLEO ikipatikana irudishwe kwa MKURUGENZI WA HALMASHAURI YA MJI KOROGWE WA S.L.P 615, KOROGWE.

Nyambega D. Kichele,
AFISA ARDHI MTEULE,
HALMASHAURI YA MJI KOROGWE

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO MJINI**
**ILIYOPO MOROGORO**
**TANGAZO LA KUITWA SHAURINI**

**SHAURI LA TALAKA NAMBA: 2/2023**

**MDAI: JESCA GIFT SUDDY**
**MDAIWA: ZAWADI HAJIRI THABITI**

**KWA: ZAWADI HAJIRI THABITI**
**DAR ES SALAAM**

**Ombi la mdai JESCA GIFTSUDDY**

**Madai ya TALAKA NA MGAWANYO WA MALI**
Unatakiwa kuhudhuria hapa Mahakamani katika shauri tajwa hapo juu bila kukosa. Shauri limepangwa kusikilizwa mnamo tarehe 4 mwezi wa 5 mwaka 2023 saa 2:30 Asubuhi/alasiri.
Angalia kama hukuudhuria/hamkuudhuria siku iliyotajwa hapo juu Mahakama ikithibitisha kama umwpokea/mmepokea kuitwa shaurini, hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa/mmeshindwa.
Hati hii imetolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe 25/4/2023

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO MJINI
MOROGORO

**FORM NO. 58**
**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF BUNDA DISTRICT AT BUNDA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION COUSE NO 5 OF 2023**
**IN THE MATTER OF THE ASTETE OF THE LATE**
**ZAKAYO MILALI KATYETYE**
**AND**
**IN MATTER OF APPLICATION FOR LATTERS OF ADMINISTRAION OF ESTATE BY**
**MIRAMBO ZAKAYO KATYETYE**
**GENERAL CITIATION**
**(Rule 75)**

**All persons** claiming to have any interest in the estate of above named deceased are hereby cited to come and to see the proceedings if they think fit before the grant of matters of administration is made to the above named petitioner.

The matter cames for mention on the 19 day of MAY 2023 bafore B.C, Sokanya Story at ......
Dated at Bunda tis 19Day of April 2023


HON. ........
RESIDENT MAGISTRATE
DISTRICT COURT
BUNDA

## KUPOTEA KWA CHETI



WITNESS ZAKARIA MSOMBE anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index number S2547-0073 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia LYANDEMBELA SEKONDARI mwaka 2017. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: DAR/MAG/RB/137926/2023.

## KUPOTEA KWA CHETI



AHMADI ABDULRAHIMU anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index number S0922-0031 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia MWINYI SEKONDARI mwaka 2007. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: DAR/KIL/RB/143097/2023.

## KUPOTEA KWA VYETI



GEOFRED GABRIEL anatangaza kupotea kwa vyet vya taaluma; cheti cha kidato cha nne chenye index namba S4424-0029 kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia BUTENGORUMASA SECONDARY SCHOOL 2013, cheti cha kidato cha sita chenye index namba S0488-0557 kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia RUTABO SECONDARY SCHOOL mwaka 2016 na transcript na cheti cha chuo cha BACHELOR OF ARTS WITH EDUCATION chenye usajili namba 2016-04-05045 kilichotolea na chuo cha UDSM-DUCE mwaka 2019. Kwa yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA: GEI/CHA/RB/131990/2023

**Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0677020701**

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

Ndugu **MARWA MASANDA WAMBURA** anatangaza kupotelewa na kadi yake ya gari aina ya Toyota Raum yenye namba za usajili **T 462 DFM.** Ametoa taarifa polisi na kupewa namba **MOR/MOR/RB/144109/2023.** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# HADITHI

# MAITI KWENYE KIROBA-6

**Na Adam Fungamwango : (0716 350534)**

MBWA mmoja wa jirani wa maeneo ya Kinondoni Msisiri, alionekana kuvutiwa na kiroba kilichotupwa upenuni mwa nyumba moja. Ni moja kati ya viroba ambavyo hutupwa usiku au alfajiri na vijana wanaokusanya taka kwenye nyumba za watu na kupewa ujira kidogo. Wao badala ya kwenda kutafuta maeneo ya kutupa, hupita vichochoroni na kama hajaonekana anautupa mzigo na kuendelea na safari yake. Ilitokea kwenye nyumba moja huko, na mbwa huyo alipouvuta, viungo vya mwili wa binadamu vilianguka. Majirani wa kwanza kuona walipiga kelele na watu wakajazana. Akinamama wakiangua vilio. Viungo vilihifadhiwa kwa kufunikwa. Polisi walianza msako. Kwa kuanzia tu wakaanza kuwakamata wazoa taka na waokota chupa za kwenda kuuza, wote wa maeneo hayo na jirani wanaofahamika tayari kwa mahojiano na uchunguzi, wakihisiwa kuwa huenda mmoja wao au zaidi kuhusika na mauaji. Ni maiti ya nani? Na Muuaji ni nani? Fuatilia mwanzo hadi mwisho kujua mkasa mzima ulivyokuwa.




"Tunaweza, lakini ama tunaweza kuchukua muda mrefu sana, au tusimpate kabisa muuaji. Kama hakupatikana kwa hawa waokota makopo na wazoa taka, basi inabidi kazi ya ziada ifanyike.

Kama siyo hawa, basi muuaji atakuwa mtu ambaye anayeifahamu kazi yake vema, ambaye atakuwa amefanya hivi kwa makusudi kutengeneza mazingira ya kutuaminisha sisi askari polisi kuwa hawa vijana ndiyo wamefanya mauaji haya."

Kwa mara ya kwanza Moses na Ben, wakatikisa kichwa kwa pamoja kukubaliana na anachoongea bosi wao.

"Tuombe Mungu tumpate kati yao, lakini tukimkosa, basi kazi hii itakuwa ngumu zaidi na itahitaji mtaalam zaidi."

"Kwa nini umefikiria hivyo afande?"

"Ni kwamba siyo kama sisi hatutoweza, ila muda unaweza kuwa mrefu mno, na pia tunaweza kuumiza watu wengi ambao hawahusiki.

Hivi afande Moses, naweza hapa kukutuma kwenda kumkamata yule mama Miraji na mumewe kuwa wanahusika unaweza kukubali hilo? Kukubali unaweza kukubali kwa sababu ni amri ya mkubwa wako, je unaweza kuamini?" Swali hilo nusura limchekeshe afande Moses.

Akamkumbuka mama Miraji, mwanamke mcheshi matata ambaye alikutana naye na kumhoji, akifuatiliwa kesi huu.

"Kwangu mimi afande sidhani."

"Kwa nini?"Akauliza inspekta Frank.

"Kwanza haiwezekani mtu na mumewe wote wamuue mtu mmoja, tena mwanamke. Halafu siyo kumuua tu, wamkatekate viungo, mmh, hapana." Inspekta Frank akaangua kicheko.

"Ndiyo maana nimeona hapa tunapoendea kila mmoja tutamuona anahusika na mauaji haya, hivyo tumuongeze mtu mmoja mwenye utaalam zaidi yenu nyinyi."

"Sawa, haina neno afande, atatoka hapa hapa kwenye Jeshi la Polisi?"

"Kwetu sisi hapa nyinyi peke yenu wawili mnatosha. Nchi hii ina idara nyingi za kuilinda nchi na wananchi wake, hivyo wiki ijayo nitakuja kuwatangazia ni nani nimemuongeza na ametoka wapi. Nadhani hiyo inaweza kutusaidia kwenye hili kwa sababu wananchi kila kukicha wamekuwa wakifuatilia vyombo vya habari kutaka kujua tumefikia wapi kwenye tukio lile baya la mauaji ya binti yule, Tessy."

**"Oooh! Karibu sana rafiki yangu, nimefurahi sana kukuona."**

*****************************************

Alikuwa ametoka usingizini na sasa alijinyoosha akipiga miayo. Alijitazama kwenye kioo akatamasamu. Nusu lilikuwa halisi, lakini nusu siyo. Alijiona amenenepa. Kunenepa kwa mtu wa kawaida ilikuwa ni furaha kwake. Hata kama hakuwa na kipato kikubwa lakini watu wanamsifia na kudhani huenda siku hizi pesa zimemtembelea.

Kwa hali ya kawaida kwa wengi kunenepa ni tunu na ni dalili za mafanikio, afye njema na maisha kuendela vizuri. Lakini siyo kwake.

Hakuupenda unene. Alipenda awe kwenye hali ya kawaida kwanza kutokana na kazi yake, halafu pia muonekano.

Ni mwezi wa pili sasa hakufanya mazoezi yoyote ya maana. Ni kwa sababu kwa muda mrefu hajafanya kazi yoyote ambayo ingemchangamsha.

Alichukua gazeti la nipashe na kuanza kusoma. Moja kati ya habari zilizomvutia ni za maendeleo ya tukio la kuuawa mwanamke mmoja mke alitwaye Tessy miezi miwili iliyopita.

Kutokana na kazi yake, alipenda sana kusoma matukio ya aina hiyo. Kwenye habari hiyo ni kwamba Jeshi la Polisi lilikuwa likiwatoa hofu wananchi kuwa muuaji au wauaji wa mwanamama huyo atapatikana hivi karibu kwani wamefikia sehemu nzuri.

Wakati akimalizia, siku yake ya mkononi iliita. Ilikuwa mezani. Alichukua na kuangalia namba. Akatabasamu, "nini tena?" Akajiuliza.

Kwake haikuwa kawaida kuitwa na mtu huyo ingawa wanafahamiana.

Baada ya salamu, akamwambia, "nakuhitaji ofisi kwangu leo hii mwamba, kumbuka ni muhimu sana."

"Poa, basi ngoja nitokea hapa, niende ofisini nikaweke mambo yangu vizuri, halafu nitafika huko."

Aliingia kwenye gari yake aina ya Bentley na kuendesha taratibu, akiliacha eneo analoishi ya Kijitonyama, Dar es Salaam kuelekea ofisi kwake maeneo ya Posta Mpya.

Dakika 15 tu baadaye alitoka na kuingia tena kwenye gari, sasa akielekea alikoitwa.

********************************

"Oooh! Karibu sana rafiki yangu, nimefurahi sana kukuona."

"Ahsante sana, nami pia, maana muda sasa."

"Ni kweli unajua tena kazi zetu hizi, ukiona kimya ujue mambo safi, ukiona simu ujue kumekucha." Wakacheza kwa pamoja.

Mgeni akajikaribisha mwenyewe kwenye kiti.

Hakuwa mwingine ila ni Inspekta Frank. Aliamua kwa dhati kumuongeza mtu ambaye alikuwa na hakina kuwa anaweza kuifanya kazi hii kwa ufanisi mkubwa.

Mtu ambaye taifa linamtegemea kwa kesi kubwa za kipelelezi ndani ya nje ya nchi. Amefanya nyingi, lakini za kukumbukwa na hasa za ndani ni zile ambazo zilisimuliwa kwenye hadithi zilizotoka kwenye gazeti la Nipashe 'Mauaji Harusini', 'Muuaji ni Nani', 'Kisanduku Cheusi' na zingine nyingi ambazo alipeleleza kupata wahusika waliofanya matukio ambao walitumia nguvu kubwa na gharama kujilinda, ikiwemo hata kuajiri watu wenye uwezo mkubwa wa sanaa za mapigano.

Lakini kwa mwamba huyu walishinda na wahusika walipatikana na sasa wanatumikia kifungo. Huyu si mwingine ila ni Eddy Kamal.

"Bwana Kamal, mimi nimekuita hapa kwa kazi moja tu. Kwetu imekuwa ngumu, lakini mimi ninavyokujua na historia ya nchi hii inavyokutambua, haitokuwa ngumu kwako.

Nadhani umeshasikia miezi miwili iliyopita kumetokea mauaji ya dada mmoja hivi anaitwa Tessy. Huyu aliuawa na kukatwakatwa viungo vyake vitatumbukizwa kwenye kiroba na kutupwa maeneo ya Kinondoni Msisiri. Tumehangaika sana, ikiwa ni pamoja na kuwakamata washukiwa ambao ni waokota makopo ya plastiki pamoja na wazoa taka. Cha ajabu ni kwamba watano baada ya kuwatikisa kidogo watano wamekiri kufanya tukio hilo, lakini baadaye tukaja gundua kuwa walikiri kwa sababu ya kibano kwa sababu kila mmoja anasema aliua yeye. Wengine tumewaachia, tumewabakisha hao watano, labda tunaweza kupata mmoja kati hao."

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

# PLUIJM AJIPANGA KUTIBUA MIPANGO YA YANGA BARA

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Singida Big Stars, Hans Pluijm, amesema anajipanga kuharibu mipango ya Yanga baada ya kubaini idara wanayoitegemea katika kupata ushindi watakapokutana kwenye michezo miwili itakayochezwa hivi karibuni kwenye Uwanja wa CCM LITI ulioko mkoani, Singida.

Singida Big Stars itaikaribisha Yanga katika mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara utakaochezwa Mei 4, mwaka huu na siku tatu baadaye watakutana kwenye mechi ya hatua ya nusu fainali ya mashindano ya Kombe la FA (ASFC).

Akizungumza na NIPASHE jana, Pluijm alisema atahakikisha kikosi chake hakifanyi makosa katika michezo hiyo miwili na kuishangaza Yanga.

Pluijm alisema anafahamu Yanga wana umahiri mkubwa katika kutumia nafasi wanazozitengeneza na anakiandaa kikosi chake kukabiliana na hali hiyo, ikiwezekana kuvuruga mipango yao ndani ya dakika zote 90.

"Nimekuwa nikiwafuatilia Yanga katika michezo ya ligi na michuano ya kimataifa, nimewaona wapinzani wangu ni wazuri katika kutumia makosa na kufutafuta ushindi. Hatuwezi kurudia makosa ya nyuma, tupo kwenye nusu fainali, katika mpira kila kitu kinawezekana na hakuna kinachoshindikana, pale utakuwa unaamini unaweza kufanya kitu ndani ya timu yako," alisema Pluijm.

Kocha huyo alisema aliongeza maandalizi ya kikosi yanaendelea vizuri na wanahitaji kufanya vizuri katika yote ili watimize malengo yao.

"Bado tuna nafasi ya kuweka rekodi na historia, tuna kikosi chenye wachezaji wazoefu na wenye kiu ya mafanikio, hatutabweteka, tutapambana kwa dakika zote, tunahitaji kusonga mbele kwenye FA na kujiimarisha katika ligi," aliongeza kocha huyo.

Alisema wanafahamu mechi zote ni ngumu na kila timu inahitaji kupata ushindi ili kujiondolea presha katika kufikia malengo.

Yanga ndio mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara na pia wanashikilia Kombe la FA.



Mshambuliaji wa Timu ya vijana ya Simba (kulia), akijiandaa kumtoka nyota wa Ihefu katika mechi ya Ligi ya U-17 ya Shirikisho la Soka Tanzania (TFF) inayoendelea jijini, Dar es Salaam. Timu hizo zilitoka sare ya mabao 2-2. **PICHA: TFF**

# JKT Tanzania yajiweka sawa

**Na Saada Akida**

BAADA ya kufanikiwa kurejea katika Ligi Kuu Bara, uongozi wa JKT Tanzania FC umesema umeshaanza mikakati ya kuimarisha kikosi chao kwa ajili ya kufanya vyema katika msimu ujao.

JKT Tanzania imeweka wazi itafanya maboresho katika utawala, benchi la ufundi na kusajili wachezaji wapya ambao watasaidia timu kupambana na ushindani wa mechi za Ligi Kuu Bara.

Akizungumza na NIPASHE jana, Katibu Mkuu wa JKT Tanzania, Abdul Nyumba, alisema kama walivyofanya maandalizi wakati wanashiriki Ligi ya Championships ndio watafanya kuelekea msimu ujao na wanaamini watakuwa imara.

Nyumba alisema wataweka nguvu zaidi katika kikosi chao kwa kufuata ushauri wa benchi la ufundi linaloongozwa na Hamsini Malale.

"JKT Tanzania sio wageni katika Ligi Kuu na sasa tumerejea tena, tutakuja kivingine kabisa, tumeshaamza kujiimarisha kwenye utawala na suala la benchi la ufundi tunasubiri ripoti ya kocha wetu Malale. Kuhusu kocha, bado tunahitaji kuendelea naye kwa sababu amefanikisha timu yetu kupanda Ligi Kuu, hatuwezi kumwacha, lakini tutamsikiliza kana naye atahitaji kuendelea nasi au amepata ofa sehemu nyingine," alisema Nyumba.

Aliongeza katika usajili wa wachezaji watazingatia nidhamu na viwango vya nyota husika ili kuhakikisha hawashuki tena daraja.

## New Generation na hesabu za CECAFA

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

MABINGWA wa Ligi Kuu ya Wanawake Zanzibar, New Generation Queens wanatarajia kuanza maandalizi kwa ajili ya kufanya vizuri katika mashindano ya Afrika Mashariki na Kati, yatakayofanyika hivi karibuni ya Cecafa.

Simba Queens ya Tanzania Bara ndio mabingwa watetezi wa mashindano hayo yatakayofanyika kuanzia Agosti 12 hadi 26, mwaka huu nchini Uganda.

Kaimu Katibu Msaidizi wa timu hiyo, Hafidha Juma, alisema wamepanga kuanza mazoezi mapema ili kujiimarisha kwa ajili ya kwenda kupeperusha vyema bendera ya Zanzibar katika michuano hiyo.

Hafidha alisema mipango waliyojiwekea uongozi wa timu hiyo ni kufanya usajili mzuri utakaopelekea kutimiza malengo yao ya kufanya vizuri mwaka huu.

"Msimu huu tumedhamiria kufanya vizuri, na ili tufanye vizuri lazima tusajili wachezaji wenye viwango vinavyoendana na mashindano hayo, " alisema kiongozi huyo.

## MeridianBET waja na Blackjack Live

**Na Saada Akida**

KATIKA kuhakikisha wanaongeza wigo kwa wadau wao wa soka, Kampuni ya MeridianBet imetambulisha mchezo mpya wa Blackjack Live, imeelezwa.

Mkuu wa Kitengo cha Masoko na Mawasiliano wa Meridianbet Tanzania, Martin Nkurlu, alisema jana kampuni yao imekuja na jambo jipya ambalo kwa sasa ni mchezo unaopendwa na kuchezwa sana ulimwenguni.

Nkurlu alisema Kasino ya Mtandaoni ya Meridianbet kwa kushirikiana na Expanse Studios wamekuja na sloti ya kijanja ya Blackjack Live ambao ni mchezo wa karata yenye maudhui na sheria za Ulaya unaochezeshwa mubashara kwa kutumia kibunda chenye karata nane.

"Unachotakiwa kukifanya ni kubashiri karata gani mchezeshaji ataiweka mezani na kuifunua. Tofauti ya Blackjack Live na Blackjack nyingine, hii ina bunda lenye karata nane na sio 52, mchezo huu unachezwa mubashara kabisa kutoka kwenye studio za Riga," alisema Nkurlu.

Aliongeza chaguo la Bet Behind litampa fursa mchezaji kuweka dau hata kama atachelewa kuanza na mchezeshaji atasaidiwa namna anayotakiwa kufanya kwenye mchezo huo.

## ZISIKUPITE

### MADRID YAMFUATA JUDE

MAOFISA wa Real Madrid watasafiri hadi Ujerumani wiki hii katika jitihada za kumshawishi kiungo wa kati wa Borussia Dortmund na England, Jude Bellingham, mwenye umri wa miaka 19 ili kujiunga na klabu hiyo ya Hispania msimu huu wa joto. (***Mara***)

### RICE AKARIBIA ARSENAL

KIUNGO wa kati wa West Ham na Timu ya Taifa ya England, Declan Rice, mwenye miaka 24, yuko kileleni mwa orodha ya wachezaji wanaolengwa na Arsenal msimu huu wa joto. (***Telegraph***)

### TUCHEL AMTAKA CASEMIRO

KIUNGO wa kati wa Manchester United na Timu ya Taifa ya Brazil, Casemiro mwenye umri wa miaka 31, ananyatiwa na Thomas Tuchel katika klabu ya Bayern Munich msimu wa joto. (***Kicker***)

### KOVACIC ANUKIA BAYERN

KOCHA wa Bayern Munich, Thomas Tuchel pia anataka kuungana tena na kiungo wa kati wa Chelsea na Timu ya Taifa ya Croatia, Mateo Kovacic, mwenye umri wa miaka 28. (***Sport1***)

### BAYERN: GREVENBERCH HAUZWI

BAYERN Munich haina nia ya kumuuza kiungo wa kati wa Uholanzi, Ryan Gravenberch, mwenye umri wa miaka 20 msimu huu, licha ya klabu za Liverpool, Manchester United na Arsenal kuonyesha nia kutaka kumsajili nyota huyo. (***Caught-Offside***)

### NAGELSMANN BEI JUU

KOCHA wa zamani wa Bayern Munich, Julian Nagelsmann, yuko kileleni mwa orodha ya makocha wanne walioteuliwa kukaribia kutua Tottenham Hotspur lakini Mjerumani huyo mwenye umri wa miaka 35, anaweza kuwa ghali sana. (***Telegraph***)

### TONEY ATAJWA VILLA

KLABU ya Aston Villa inapania kumnunua mshambuliaji wa Brentford na na Timu ya Taifa ya England, Ivan Toney, mwenye umri wa miaka 27. (***Football Insider***)

### FELIX KUBAKIA CHELSEA

MSHAMBULIAJI wa Timu ya Taifa ya Ureno, Joao Felix, hatarejea Atletico Madrid msimu wa joto, huku mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23 akitarajiwa kuongeza mkataba wake wa mkopo na Chelsea. (***Sun***)

### MILAN YAMFUATA NELSON

AC Milan wanafuatilia hali ya winga wa Arsenal, Reiss Nelson, mwenye umri wa miaka 23, ambaye bado hajasaini mkataba mpya. (***Calciomercato***)

### LOFTUS-CHEEK SOKONI

AC Milan pia inavutiwa na kiungo wa kati wa Chelsea na Timu ya Taifa ya England, Ruben Loftus-Cheek, mwenye umri wa miaka 27. (***90min***)

### VANDERSON ANUKIA UNITED

MANCHESTER United inatayarisha ofa ya kumnunua beki wa kulia wa Monaco, Mbrazil Vanderson mwenye umri wa miaka 21, lakini huenda wakakabiliwa na ushindani kutoka kwa klabu nyingine kadhaa zinazoshiriki Ligi Kuu England. (***RMC Sport***)

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# DE BRUYNE : CITY NI KUFA AU KUPONA

### Wajipanga kupambana ili kubeba mataji yote matatu kama...

**MANCHESTER,** England

KEVIN De Bruyne amedai mtazamo wa "kufa au kupona" unaifanya Manchester City kusonga mbele katika harakati zao za kutaka kutwaa mataji matatu msimu huu.

**City walichukua udhibiti thabiti wa mbio za kuwania taji la Ligi Kuu England Ju matano walipowalaza vinara Arsenal mabao 4-1 katika mechi iliyochezwa kwenye Uwanja wa Etihad.**

Ushindi huo uliwafanya wapunguze hadi pointi mbili kileleni na wakiwa na michezo miwili mkononi, wako katika nafasi nzuri ya kutwaa taji lao la tano ndani ya miaka sita.

City pia wametinga fainali ya Kombe la FA na wako katika nne bora ya Ligi ya Mabingwa Ulaya huku wakiwa na nafasi kubwa ya kuiga mafanikio ya Manchester United ya mwaka 1999 ya kunyakua mataji yote matatu.

"Nadhani tumekuwa tukicheza vyema kwa miezi kadhaa, na kushinda mechi nyingi," alisema mchezaji, De Bruyne, ambaye alifunga mara mbili katika ushindi huo dhidii ya Arsenal.

"Tumekuwa vizuri katika safu ya ulinzi hivi karibuni lakini tunajua ni kufa au kupona katika kila mechi. Itakuwa sawa Jumapili, lazima tushinde. Hatuwezi kushinda huyu halafu tuende Fulham na tusishinde.

"Nadhani kila mtu anataka kucheza katika michezo kama hii. Tumebahatika sana kucheza katika michezo hii mara nyingi, kuwa katika nafasi hii.

"Ni vizuri kupigania mambo haya. Tunaendelea hadi mwisho wa msimu."

Bao la kwanza la De Bruyne lilipatikana baada ya dakika saba pekee na pia alitoa krosi kwa John Stones kufunga bao la pili kabla ya mapumziko.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,107,4

MECHI KALI
REAL MADRID
VERSUS
ALMERIA
1 | 1.18
X | 6.35
2 | 11.47

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa
vodacom m-pesa
halopesa
airtel money
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#

GBT:0249 18+
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# SON: SPURS ILIKATAA TENA KUDHALILISHWA NA UNITED



**LONDON,** England

MCHEZAJI Heung-min Son amesema Tottenham Hotspur walijua hakungeweza kurudiwa kwa fedheha "isiyokubalika" ya St James' Park walipopambana na kutoka sare ya mabao 2-2 dhidi ya Manchester United katika mechi ya Ligi Kuu England iliyochezwa juzi.

Matumaini ya Spurs kumaliza katika nafasi nne bora kwenye Ligi Kuu England yalitikiswa na kipigo cha mabao 6-1 kutoka kwa Newcastle United Jumapili iliyopita.


Kocha wa muda, Cristian Stellini, aliondolewa majukumu yake huku Ryan Mason akichukua kiti hadi mwisho wa msimu huu.

Tottenham walionekana katika hatari ya kukumbwa na janga jingine baada ya Mashetani Wekundu kutangulia kwa mabao mawili yaliyofungwa na Jadon Sancho na Marcus Rashford, lakini walijizatiti katika kipindi cha pili na kuokoa pointi, Pedro Porro akipunguza nusu ya bao na Son kusawazisha baada ya Harry Kane kumtengenezea pande zuri.

Son alisema: "Tulitaka kutoa kila kitu na hiyo ilikuwa hotuba ya chumba cha kubadilishia nguo. Hatukuweza kuuacha mchezo uendelee. Tulikasirishwa sana na hilo, hatukustahili kuwa chini kwa mabao 2-0 hadi mapumziko.

Wiki iliyopita ilikuwa haikubaliki na hatukutaka kurudia hilo. Tunasikitika sana kwa utendaji na matokeo na tulitaka kuleta nguvu nzuri."

# *Afya ya Neymar yaimarika*




**PARIS,** Ufaransa

NEYMAR aliondolewa kiatu cha ulinzi kwenye mguu wake wa kulia siku ya Alhamisi baada ya kupokea "matokeo ya kutia moyo" kutokana na vipimo vya jeraha lake la kifundo cha mguu.

Mshambuliaji huyo wa Paris-Saint Germain alifanyiwa upasuaji mwezi uliopita baada ya kuumia wakati wa ushindi wa mabao 4-3 wa Ligue 1 dhidi ya Lille.

PSG ilifichua Neymar atatarajiwa kuwa nje ya uwanja kwa miezi mitatu hadi minne.

Viongozi hao wa Ligue 1 juzi walitoa taarifa chanya juu ya kupona kwa mchezaji huyo mwenye miaka 31.

Taarifa iliyotolewa na klabu hiyo ilisema: "Neymar Jr amerejea katika kituo cha mazoezi huku wahudumu wa afya wa Paris Saint-Germain na madaktari wa upasuaji waliomfanyia upasuaji wakimwondolea kiatu chake cha ulinzi, Baada ya kupata matokeo ya uhakika kutoka kwa vipimo vyake, mchezaji huyo sasa ataweza kuendelea na kujiuguza hapa Paris."

Neymar amekuwa akifurahia msimu wake wenye tija zaidi kwa PSG tangu msimu wa 2018-19, akifikisha jumla ya mabao 34 ya moja kwa moja (mabao 18, pasi 16) katika mashindano yote, akiwa nafasi ya pili kwa juu zaidi katika maisha yake ya soka ya PSG, nyuma ya mabao 44 aliyofunga. msimu wa kwanza.

# NAMUNGO YAANZA VITISHO IKIWAKARIBISHA SIMBA SC

**Na Shufaa Lymio**

HATUWAHOFII, hayo ni maneno ya benchi la ufundi la Namungo FC kuelekea mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Simba itakayochezwa Mei 3, mwaka huu kwenye Uwanja wa Majaliwa ulioko Ruangwa mkoani, Lindi.

Akizungumza na NIPASHE jana, Kocha Mkuu wa Namungo, Denis Kitambi, alisema kikosi chake kinaendelea na programu mbalimbali za mazoezi kwa lengo la kujiimarisha ili kusaka ushindi katika mechi hiyo.

Kitambi alisema wanafahamu ubora wa Simba na kwa sababu hiyo watacheza kwa tahadhari na kamwe hawaihofii timu hiyo ya Mtaa wa Msimbazi, Kariakoo, Dar es Salaam.

**"Tunajiimarisha, tunajipanga kumkabili mpinzani wetu ambaye tunajua anashiriki mashindano ya kimataifa, hatumhofii. Ninaamini kila kitu kitakwenda sawa," Kitambi.**

Aliongeza anaendelea kuyafanyia kazi makosa yaliyojitokeza katika michezo iliyopita kwa lengo la kumaliza msimu kwa kuzibakisha pointi nyumbani.

"Malengo yangu ni kuhakikisha timu inafamya vyema michezo yote iliyobakia, ninaomba mashabiki wetu waendelee kutupa ushirikiano," Kitambi alisema.

Aliongeza anaendelea kuwajenga kisaikolojia wachezaji ili wasicheze chini ya kiwango huku akiendelea kushukuru wanaendelea vyema kiafya.



Mashabiki wa Yanga wakichangia damu na baadaye kupewa tiketi za kushuhudia mechi ya robo fainali ya mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Rivers United kutoka Nigeria itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam. **PICHA: MTANDAO**

# Rais Samia aongeza dau

INATOKA UK 24

mbele, tunaamini msimu huu Tanzania itaweka historia na alama nzuri," Hamadi alisema.

Mdau mwingine wa soka, Amina Poyo, alisema kitendo anavyofanya Rais Samia ni cha kuwaongezea ushujaa wachezaji wetu ambao wanapeperusha bendera ya Tanzania katika mashindano hayo ya CAF.

"Ni chachu kubwa na viongozi wa klabu wanapata unafuu pindi bonasi hizo zinapopatikana, motisha hii ni kubwa sana," Poyo alisema.

Rais Samia alianza kutoa motisha hizo kuanzia hatua ya makundi na timu zimekuwa zikikabidhiwa kila wanapomaliza mchezo kwa mechi za nyumbani na wanaporejea kutoka michezo ya ugenini.

**Imeandaliwa na Saada Akida na Shufaa Lyimo.**

65,397/-

SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 29/04/23 | 19:00 | AS Roma vs AC Milan | 2.60 | 2.95 | 2.75 |
| 02. 29/04/23 | 19:30 | Schalke 04 vs Werder Bremen | 2.21 | 3.45 | 2.85 |
| 03. 29/04/23 | 20:00 | Velez Sarsfield vs CA San Lorenzo de Almagro | 2.30 | 2.80 | 3.00 |
| 04. 29/04/23 | 21:30 | Servette Geneva vs FC St. Gallen 1879 | 2.38 | 3.20 | 2.46 |
| 05. 29/04/23 | 21:45 | Torino FC vs Atalanta BC | 2.80 | 3.20 | 2.39 |
| 06. 29/04/23 | 22:30 | Gimnasia Y Esgrima La Plata vs CA Tigre | 2.70 | 2.95 | 2.33 |
| 07. 29/04/23 | 22:30 | Coritiba FC PR vs Sao Paulo FC SP | 2.95 | 3.10 | 2.34 |
| 08. 29/04/23 | 22:30 | Fortaleza EC CE vs Fluminense FC RJ | 2.60 | 3.15 | 2.60 |
| 09. 30/04/23 | 14:00 | Skovde AIK vs IK Brage | 2.70 | 3.10 | 2.25 |
| 10. 30/04/23 | 15:00 | Cadiz CF vs Valencia CF | 3.00 | 3.15 | 2.29 |
| 11. 30/04/23 | 15:30 | Glasgow Rangers vs Celtic Glasgow | 2.75 | 3.15 | 2.25 |
| 12. 30/04/23 | 16:00 | AFC Bournemouth vs Leeds United | 2.65 | 3.25 | 2.48 |
| 13. 30/04/23 | 16:00 | Clermont Foot 63 vs Stade Reims | 2.90 | 3.40 | 2.23 |
| 14. 30/04/23 | 18:30 | VfL Wolfsburg vs FSV Mainz | 2.26 | 3.40 | 2.85 |
| 15. 30/04/23 | 19:00 | Besiktas Istanbul vs Galatasaray Istanbul | 2.46 | 3.20 | 2.36 |
| 16. 30/04/23 | 19:00 | Ajax Amsterdam vs PSV Eindhoven | 2.20 | 3.25 | 2.75 |
| 17. 30/04/23 | 19:30 | Espanyol Barcelona vs Getafe CF | 2.31 | 2.95 | 3.15 |

MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAMOSI - 29/04/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 5373 | Zorya Lugansk vs Chernomorets Odessa | 1.49 | 3.96 | 5.35 |
| 14:00 | 1921 | Osters IF vs Ostersunds | 1.62 | 3.95 | 5.01 |
| 14:00 | 5648 | FC Ingulets vs SC Dnipro 1 | 5.76 | 4.06 | 1.45 |
| 14:00 | 5779 | Lahti vs Inter Turku | 3.53 | 3.28 | 1.92 |
| 16:00 | 1198 | Jonkopings Sodra vs Vasteras SK | 2.81 | 3.34 | 2.41 |
| 16:00 | 1435 | Bloemfontein Celtic vs Cape Town City | 2.44 | 3.02 | 2.87 |
| 16:00 | 3661 | Napoli vs Salernitana | 1.25 | 5.24 | 9.94 |
| 16:00 | 5215 | Moreirense vs Tondela | 1.67 | 3.60 | 4.59 |
| 16:30 | 1598 | Union Berlin vs Bayer Leverkusen | 2.85 | 3.20 | 2.35 |
| 16:30 | 1811 | Eintracht Frankfurt vs Augsburg | 1.52 | 4.19 | 5.19 |
| 16:30 | 4412 | Akhmat Grozny vs CSKA Moscow | 3.15 | 3.36 | 2.11 |
| 16:30 | 4850 | FC Koln vs SC Freiburg | 2.32 | 3.20 | 2.90 |
| 16:30 | 5693 | RB Leipzig vs Hoffenheim | 1.38 | 4.72 | 6.42 |
| 16:30 | 5719 | Stuttgart vs Monchengladbach | 1.79 | 3.71 | 3.81 |
| 17:00 | 4065 | Stoke City vs QPR | 1.91 | 3.41 | 3.66 |
| 17:00 | 4869 | HK Kopavogs vs Fylkir | 2.17 | 3.73 | 2.70 |
| 17:00 | 5113 | Brighton vs Wolverhampton | 1.47 | 4.20 | 5.80 |
| 17:00 | 5156 | AL Arabi vs Hatta Club | 2.93 | 3.44 | 2.09 |
| 17:00 | 5855 | Brentford vs Nottingham | 1.61 | 3.70 | 5.01 |
| 17:15 | 3506 | Elche vs Rayo Vallecano | 4.50 | 3.45 | 1.73 |
| 17:30 | 1290 | Maritimo vs Vitoria Guimaraes | 2.47 | 3.15 | 2.75 |
| 17:30 | 4151 | Sporting Braga vs Portimonense | 1.24 | 5.61 | 9.82 |
| 18:00 | 4001 | WSG Wattens vs TSV Hartberg | 2.04 | 3.39 | 3.08 |
| 18:00 | 4901 | Maktaaral vs Ordabasy | 3.99 | 3.26 | 1.84 |
| 18:00 | 5766 | Lille vs AC Ajaccio | 1.20 | 5.80 | 11.99 |
| 18:00 | 5834 | Josko Ried vs Austria Lustenau | 2.04 | 3.28 | 3.18 |
| 18:30 | 4114 | Maccabi Netanya vs FC Ashdod | 2.23 | 3.13 | 2.93 |
| 18:30 | 4634 | Wisla Krakow vs Chojnice | 1.40 | 4.23 | 6.19 |
| 18:30 | 4837 | Stellenbosch vs Golden Arrows | 2.26 | 3.04 | 3.15 |
| 19:00 | 2394 | FC Krasnodar vs Ural Yekaterinburg | 1.84 | 3.56 | 3.77 |
| 19:00 | 3773 | Sivasspor vs Fenerbahce | 3.99 | 3.68 | 1.78 |
| 19:00 | 3991 | Roma vs AC Milan | 2.66 | 2.91 | 2.71 |
| 19:00 | 4130 | Ankaragucu vs Kasimpasa | 2.06 | 3.47 | 3.21 |
| 19:00 | 4434 | Bodo Glimt vs Brann | 1.75 | 3.83 | 3.94 |
| 19:30 | 3304 | West Bromwich vs Norwich City | 2.03 | 3.35 | 3.35 |
| 19:30 | 3722 | Real Madrid vs Almeria | 1.18 | 6.35 | 11.47 |
| 19:30 | 4029 | Spartak Moscow vs Rostov | 1.69 | 3.87 | 4.19 |
| 19:30 | 5563 | Schalke 04 vs Werder Bremen | 2.24 | 3.40 | 2.85 |
| 19:30 | 5892 | Albacete Balompie vs FC Cartagena | 2.08 | 3.19 | 3.39 |
| 20:00 | 3331 | FC Vizela vs Pacos Ferreira | 1.81 | 3.37 | 4.23 |
| 20:00 | 5483 | GD Chaves vs Casa Pia Atletico | 2.24 | 3.16 | 3.11 |
| 20:30 | 3503 | Al Hilal Riyadh vs Urawa Red Diamonds | 1.95 | 3.43 | 3.38 |
| 21:00 | 2738 | Amazulu vs Sekhukhune United | 2.46 | 2.78 | 3.10 |
| 21:45 | 2965 | Torino vs Atalanta | 2.80 | 3.19 | 2.39 |
| 22:00 | 1379 | Tenerife vs Leganes | 2.00 | 2.96 | 3.97 |
| 22:00 | 1699 | Nantes vs Toulouse | 2.83 | 3.34 | 2.37 |
| 22:00 | 2802 | Barcelona vs Betis | 1.37 | 4.53 | 7.22 |
| 22:30 | 4417 | Gil Vicente vs Benfica | 7.83 | 5.22 | 1.31 |
| 22:30 | 5296 | Fortaleza CE vs Fluminense | 2.61 | 3.15 | 2.51 |
| 22:30 | 5658 | Coritiba vs Sao Paulo | 2.92 | 3.07 | 2.32 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

Michezo
Nipashe Jumamosi Aprili 29, 2023



De Bruyne : City ni kufa au kupona
UKURASA 21

# Rais Dk. Samia aongeza dau

## ●●● Sasa kununua kila bao la Simba, Yanga nusu fainali kwa Sh. milioni 10...



Kiungo wa Yanga, Mudathir Yahaya. **PICHA: MAKTABA**

**Na Waandishi Wetu**

KAZI kwenu, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan, ameongeza kiasi cha fedha za motisha kwa timu za Simba na Yanga ambazo zinashiriki mashindano ya kimataifa yanayoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF), imeelezwa.

**Simba jana usiku iliku wa dimbani inacheza mechi yake ya hatua ya robo fainali ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya wenyeji Wydad AC ya Morocco wakati Yanga inayoshiriki michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika itawakaribisha Rivers United kesho kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.**

Msemaji Mkuu wa Serikali, Gerson Msigwa, alisema jana, Rais Samia, sasa ameahidi kutoa Sh. milioni 10 badala ya Sh. milioni tano kwa kila goli litakalofungwa na wachezaji wa timu hizo endapo watafuzu kucheza hatua ya nusu fainali ya mashindano hayo ya CAF.

Hata hivyo, Msigwa alisema magoli yatakayolipiwa motisha ya Sh. milioni 10 ni yale yatakayofungwa katika dakika 90 za mchezo au dakika 120 na si kwa timu itakayokwenda hatua ya penati ili kupata klabu itakayosonga mbele.

Alisema pia kiongozi huyo mkuu wa Tanzania amezitakia mafanikio timu hizo mbili zinazopeperusha bendera ya nchi katika mashindano hayo ya kimataifa yanayofanyika kila mwaka.

"Mh. Rais Samia anazitakia kila la kheri Simba na Yanga na amewataka wachezaji kujituma uwanjani na kutumia maarifa yao yote kuhakikisha wanashinda michezo ya kukamilisha robo fainali ili wafanikiwe kuingia nusu fainali ambapo kila goli litakuwa Sh. milioni 10," alisema Msigwa.

Simba ilishuka dimbani ugenini ikiwa na mtaji wa ushindi wa bao 1-0 walioupata katika mchezo wa kwanza wa robo fainali uliochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa wiki iliyopita, bao hilo pekee likifungwa na mshambuliaji wao kutoka Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC), Jean Baleke.

Kwa upande wa Yanga ambao watacheza mchezo wa marudiano nyumbani watashuka dimbani wakiwa na mtaji wa ushindi wa mabao 2-0 waliovuna ugenini katika Mji wa Uru, ulioko Nigeria.

"Unapojua kuna kitu kimetolewa unaongeza nguvu na kujituma zaidi uwanjani. Rais Samia ameonyesha kujitoa kwake lakini anapenda michezo, hasa mpira wa miguu. Hiki kitu kilikuwa hakifanyiki huko nyuma, alianza awali na sasa ameongeza dau, tunaomba kiendelee," alisema Ambangile ambaye ni shabiki wa Wekundu wa Msimbazi.

Henry Ambangile, mdau wa soka hapa nchini alisema kitendo cha kutoa motisha kwa timu hizi kongwe kinaleta motisha kwa wachezaji na kinaongeza hamasa ya kufanya vizuri katika kila mechi wanayocheza.

Naye shabiki wa Yanga, Sudi Hamadi, aliliambia gazeti hili motisha zinazotolewa ni mwendelezo wa neema kwa timu za Tanzania kufanya vizuri katika mashindano hayo ya kimataifa msimu huu.

Hamadi alisema anaamini wachezaji na viongozi watahakikisha wanaendelea kumpa heshima Rais Samia na hatimaye Tanzania kuweka historia nyingine mpya katika michuano hiyo.

"Tunahitaji kuendelea kushuhudia mechi kubwa zikifanyika kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, siri kubwa ya kupata michezo hiyo kwa kuziona klabu kubwa Afrika ni kusonga

INAENDELEA UK 23

## Yanga yatamba haizuiliki Afrika

**Na Saada Akida**

HUKU wakiwa mbele na mabao 2-0, Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, amesema anakiamini kikosi chake kitafanya vizuri katika mechi ya marudiano ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Rivers United na hatimaye kusonga mbele kwenye mashindano hayo.

Nabi aliliambia NIPASHE wachezaji wake wako tayari kwa mechi hiyo na ubora wa kikosi chake unampa nafasi nzuri ya kutowahofia wapinzani wao.

Kocha huyo alisema amewataka wachezaji wake kupambana kusaka ushindi na kusahau mtaji wa mabao mawili waliopata kwenye mechi ya kwanza na kuifanya kazi yao kuwa nyepesi.

"Tumejipanga kupambana kusaka ushindi, tunataka kuendelea kufanya vizuri katika mashindano ya CAF, tunajua si kazi rahisi sana na tunaelewa mchezo wa Jumapili ni kama fainali, tutaingia tukihesabu hatuna goli lolote mkononi," alisema Nabi.

Aliongeza malengo yao bado hayajatimia ingawa wanaona njia ni nyeupe kwa upande wao na mafanikio waliyonayo mpaka sasa yanatokana na ushirikiano mkubwa uliopo kutoka kwa uongozi, benchi la ufundi, wachezaji na mashabiki wa timu hiyo.

"Licha ya kufanya vizuri bado wachezaji hawatakiwi kujiamini kuwa tumemaliza kazi, wanatakiwa kusahau matokeo ya mechi ya kwanza na kuongeza nguvu katika mechi ya Jumapili," alisema kocha huyo raia wa Tunisia.

Aliongeza wataingia uwanjani huku wakiwaheshimu wapinzani wao kwa sababu katika mpira lolote linaweza kutokea.

"Ninasisitiza kuongeza umakini na kujitoa katika muda wote wa mechi, ni lazima wachezaji wajitoe katika kila mechi hasa za kimataifa ili kuiona Yanga ikijijengea heshima na kuwa tishio kimataifa.

Furaha ya ushindi iliishia huko Nigeria, hapa tumekuja kuanza upya na kuhakikisha tunawaondoa Rivers United, hatutakiwi kuwadharau, tusiamini utakuwa mchezo rahisi, hakuna kitu chepesi," alisema Nabi.

Aliongeza mechi ya kesho itakuwa tofauti na ile ya kwanza kwa sababu wachezaji wameshajuana na wanajua Rivers United watashuka dimbani kivingine kwa sababu ya kusaka ushindi kama waliopata wao wakiwa Nigeria.



9 770856 541002 >